



2020/21

# HOTUBA YA BAJETI WIZARA YA NISHATI

**HOTUBA YA WAZIRI WA NISHATI MHE. DKT.  
MEDARD MATOGOLO CHANANJA KALEMANI (MB.),  
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA  
MATUMIZI YA WIZARA YA NISHATI KWA MWAKA 2020/21**



**Waziri wa Nishati, Mheshimiwa  
Dkt. Medard Kalemami**



**Naibu Waziri wa Nishati,  
Mheshimiwa Subira Mgalu**



**Katibu Mkuu wa Wizara ya  
Nishati, Mhandisi Zena Said**



**Naibu Katibu Mkuu wa  
Wizara ya Nishati, Mhandisi  
Leonard Masanja**

## A. UTANGULIZI

1. *Mheshimiwa Spika*, kutokana na Taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka 2019/20 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake kwa Mwaka 2020/21.

2. *Mheshimiwa Spika*, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uzima na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu leo kutoa taarifa ya utekelezaji wa Serikali kupitia Sekta ya Nishati. Namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuendelea kuwajalia afya njema Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa, Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, Waheshimiwa Wabunge na Viongozi wengine mbalimbali.

3. *Mheshimiwa Spika*, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo yake thabiti yanayoniwezesha kuisimamia vema Sekta ya Nishati. Ni dhahiri kuwa Rais wetu amekuwa chachu katika kutekeleza mipango mikubwa na yenye tija katika Sekta ya Nishati hapa nchini.

4. *Mheshimiwa Spika*, napenda piakuwashukuru Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo mbalimbali wanayoniwezesha kuisimamia Sekta ya Nishati. Nikiri kuwa maelekezo na miongozo ya viongozi wetu hawa ni msingi wa mafanikio ya utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Nishati. Aidha, napenda kumpongeza Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuisimamia kwa umahiri utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

5. *Mheshimiwa Spika*, naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza Mawaziri walioteuliwa hivi karibuni na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nampongeza Mhe. George Boniface Simbachawene (Mb.), aliyeteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb.), aliyeteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano na Mazingira na Mhe. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb.), aliyeteuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Nawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yao.

6. *Mheshimiwa Spika*, nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Wenyeviti wote wa Kamati Mbalimbali za Kudumu za Bunge pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge lako Tukufu kwa utendaji kazi wenu mahiri. Napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini Mhe. Dunstan Luka Kitandula (Mb.), Makamu Mwenyekiti Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri (Mb.), na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa ushauri na maelekezo wanayotupatia katika kuboresha utendaji kazi wa Wizara.

7. *Mheshimiwa Spika*, tarehe 15 Januari, 2020, Bunge lako Tukufu lilimpoteza Mhe. Rashid Ajali Akibar, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini, tarehe 20 Aprili, 2020



Bunge lako lilimpoteza Mhe. Dkt. Getrude Pangalile Rwakatara aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (CCM), tarehe 29 Aprili, 2020 Bunge lako pia lilimpoteza Mhe. Richard Mganga Ndassa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Sumve na tarehe 01 Mei, 2020 Bunge lilimpoteza Mhe. Augustine Philip Mahiga aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria na pia Mbunge. Naungana na wabunge wenzangu kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu, familia za marehemu, ndugu, jamaa, marafiki na wote walioguswa na misiba hiyo. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

8. *Mheshimiwa Spika*, namshukuru Mhe. Subira Khamis Mgalu, (Mb.), Naibu Waziri wa Nishati kwa kunisaidia kwa karibu katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, napenda kumshukuru Katibu Mkuu Mha. Zena Ahmed Said na Naibu Katibu Mkuu Mha. Leonard Robert Masanja kwa uchapakazi wao mahiri na ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza shughuli zangu za kila siku za Wizara. Namshukuru pia aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Dkt. Hamisi Hassan Mwinyimvua kwa utumishi wake uliotukuka. Vilevile, nawashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote kwa ujumla kwa ushirikiano wao na juhudi zao wanazofanya kwa ajili ya kufanikisha malengo ya Wizara.

9. *Mheshimiwa Spika*, napenda nichukue fursa hii kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Chato kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo ya Jimbo. Wazazi wangu na wananchi wote wa Jimbo la Chato naomba mtembee kifua mbele, kijana wenu niko imara katika kuwawakilisha, na ninaahidi kuwa sitawaangusha na nitaendelea kushirikiana nanyi katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla. Naishukuru sana familia yangu ikiongozwa na Mke wangu Mama Kalemani pamoja na watoto wangu kwa kuendelea kuniombea na kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu ya kitaifa.

10. *Mheshimiwa Spika*, baada ya utangulizi huo, naomba sasa kuwasilisha Taarifa ya Mapato, Matumizi na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2019/20 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2020/21.

## **B. TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA 2019/20 NA MWAKA 2020/21**

### *Bajeti na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2019/20*

11. *Mheshimiwa Spika*, Bajeti iliyopitishwa kwa ajili ya Wizara ya Nishati pamoja na Taasisi zake kwa Mwaka 2019/20 ni jumla ya **Shilingi trilioni 2.143** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo ilikuwa **Shilingi trilioni 2.116** sawa na **asilimia 98.8** ya bajeti yote ya Wizara na Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ilikuwa **Shilingi bilioni 26.339** sawa na **asilimia 1.2** ya bajeti yote ya Wizara.

12. *Mheshimiwa Spika*, hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi bilioni 611.149**. Kiasi hicho kilichopokelewa na Wizara kinaendana na Mpango Kazi uliopo. Aidha, Serikali inaendelea kutoa fedha kulingana na Mpango Kazi na mahitaji yaliyopo.

### *Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali*

13. *Mheshimiwa Spika*, Wizara ya Nishati katika mwaka 2019/20 ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 602.06**. Kati ya makusanyo hayo, jumla ya **Shilingi bilioni 602.05** zilitarajiwa kukusanywa kupitia shughuli za mafuta na gesi asilia na **Shilingi milioni 12.0** kupitia shughuli za utawala. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020, Wizara kupitia shughuli za utafiti wa mafuta na mauzo ya gesi asilia pamoja na utawala imekusanya **Shilingi bilioni 501.06** Makusanyo hayo ni sawa na **asilimia 83.23** ya lengo.

## **C. MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2015/16 HADI 2020**

14. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha miaka mitano cha Serikali ya Awamu ya Tano, utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika sekta ya nishati umepata mafanikio makubwa mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

- (i) Kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme nchini ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 uwezo wa mitambo ya kufua umeme nchini umeongezeka na kufikia jumla ya MW 1,601.84 kutoka MW 1,308 mwaka 2015;
- (ii) Kukamilika kwa Miradi ya Kuzalisha Umeme ya Kinyerezi I MW 150 na Kinyerezi II MW 240. Ujenzi wa miradi ulikamilika kwa asilimia 100 mwaka 2016 na mwaka 2018 mtawalia, ambapo jumla ya MW 398.22 zimeingizwa kwenye Gridi ya Taifa;
- (iii) Kuendelea na Ujenzi wa Mradi wa Julius Nyerere Hydro Power Project (JNHPP) MW 2,115 ambao hadi sasa utekelezaji wake umefikia zaidi ya asilimia 85 kulingana na Mpango Kazi wa kazi zilizopangwa;
- (iv) Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Rusumo MW 80 ambao hadi sasa utekelezaji wake umefikia asilimia 61;
- (v) Kuunganisha Mikoa ya Lindi, Mtwara, Njombe na Ruvuma katika Gridi ya Taifa ambako kumewezesha kusitisha uzalishaji wa umeme kwa kutumia mitambo ya mafuta mazito ambayo ilikuwa inaigharimu TANESCO wastani wa Shilingi bilioni 15.3 kwa mwaka;
- (vi) Kukamilika kwa Mradi wa njia ya kusafirisha umeme kV 220 kutoka Makambako hadi Songea ambao ulikamilika mwezi Septemba, 2018 na kuwezesha vijiji vyote 122 kuunganishiwa umeme;
- (vii) Kuendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa kV 220 kwa ajili ya Mradi wa Treni ya Mwendu Kasi (SGR) awamu ya kwanza (Lot I) yenye urefu wa kilomita 160 kutoka Dar es Salaam hadi Kingolwira, Morogoro;
- (viii) Kuendelea na Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini



ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 jumla ya vijiji 9,112 vimeunganishiwa umeme ikilinganishwa na vijiji 2,018 vilivyokuwa vimeunganishwa umeme mwaka 2015 sawa na ongezeko la asilimia 351.54;

- (ix) Kuendelea kutokuwa na mgawo wa umeme nchini na kuwa na ziada ya umeme wa wastani wa MW 325 kwa siku;
- (x) Kuendelea na uzalishaji wa vifaa vya kujenga miradi ya umeme nchini na hivyo kusitisha uingizaji wa vifaa vya ujenzi wa miundombinu ya umeme ikiwemo nguzo, mashineumba, nyaya na mita za LUKU ndani ya nchi na hivyo kurahisisha upatikanaji wa vifaa hivyo. Uzalishaji huo pia umechangia ongezeko la ajira nchini;
- (xi) Kuunganishiwa umeme kwa wateja wapya 1,293,528 na kufanya jumla ya wateja waliounganishiwa umeme hadi mwezi Aprili, 2020 kufikia 2,766,745 ikilinganishwa na wateja 1,473,217 waliokuwepo hadi Juni, 2015 sawa na ongezeko la asilimia 88;
- (xii) Kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji wa umeme (*Overall Electricity Access rate*) nchini kutoka asilimia 67.8 mwaka 2016 na kufikia asilimia 84.6 mwaka 2020;
- (xiii) Serikali kupitia TANESCO na REA kuendelea kuunganisha umeme kwa Shilingi 27,000 katika maeneo yote ya vijijini kulingana na Mpango wa Kupeleka Umeme Vijijini;
- (xiv) Kuongezeka kwa gesi asilia iliyogunduliwa kutoka Futi za Ujazo Trilioni 55.27 mwaka 2015 na kufikia Futi za Ujazo Trilioni 57.54 mwaka 2020 sawa na ongezeko la futi za ujazo Trilioni 2.27;
- (xv) Kuimarika kwa shughuli za kaguzi za gharama katika Mikataba ya PSAs (*PSA Audit*) na hivyo kupelekea kuokoa fedha Shilingi bilioni 10.14 kwa kaguzi zilizofanyika kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2016 hadi 2018;
- (xvi) Kuanza kwa shughuli za utafutaji wa mafuta katika Kitalu cha Eyasi Wembere ambapo visima vifupi viwili (2) vyenye kina cha urefu wa mita 300 vimechorongwa katika Wilaya ya Igunga Mkoa wa Tabora na Meatu Mkoani Shinyanga;
- (xvii) Kuongezeka kwa kasi ya usambazaji wa gesi asilia ambapo katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Mtwara, jumla ya nyumba za wateja wa awali zaidi ya 1,000 zimefikishiwa miundombinu ya usambazaji gesi asilia na viwanda 48 vimeunganishwa kufikia mwezi Aprili, 2020. Aidha, zaidi ya magari 400 yamefungwa mifumo ya matumizi ya gesi asilia ikilinganishwa na magari 60 yaliyokuwa yameunganishwa mwaka 2015;
- (xviii) Kuongezeka kwa uzalishaji wa gesi asilia kutoka wastani wa futi za ujazo bilioni 37 kwa mwaka 2015 hadi futi za ujazo bilioni 46 katika mwaka 2019 sawa na ongezeko la asilimia 24;

- (xix) Kuongezeka kwa mchango wa gesi asilia katika kuzalisha umeme nchini kutoka asilimia 36 mwaka 2015 hadi asilimia 57 mwezi Aprili, 2020;
- (xx) Kuongezeka kwa ushiriki wa Watanzania katika miradi ya mafuta na gesi asilia ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2020 kampuni 457 zimeorodheshwa katika kanzidata iliyowezesha kampuni hizo kushiriki katika miradi mbalimbali;
- (xxi) Kuhuishwa kwa Bandari za Tanga na Mtwara katika kupokea Mafuta ambapo Bandari hizo zimeanza kupokea Mafuta kuanzia mwezi Julai, 2015 na Julai, 2018 mtawalia;
- (xxii) Kuendelea kuimarika kwa Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (*Bulk Procurement System – BPS*) ambao umeongeza uhakika wa upatikanaji wa mafuta nchini na kupunguza gharama za uagizaji;
- (xxiii) Kujenga uwezo katika kusimamia Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia kwa kudhamini mafunzo ya ufundi stadi kupitia vyuo vya ufundi stadi (VETA). Serikali imeendelea kutoa kozi mbalimbali zinazohusiana na mafuta na gesi katika vyuo vikuu hapa nchini kwa viwango vya Stashahada (*Diploma*), Shahada (*Bachelor*) na Uzamili (*Masters*);
- (xxiv) Kupungua kwa uchafuzi (uchakachuuji) wa mafuta kutoka wastani wa asilimia 19.2 mwaka 2015 hadi kufikia wastani wa asilimia 4 mwezi Machi, 2020.

## D. VIPAUMBELE VYA BAJETI KWA MWAKA 2019/20

**15. Mheshimiwa Spika,** maeneo ya kipaumbele ya Wizara ya Nishati kwa mwaka 2019/20 yalikuwa ni pamoja na: kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutekeleza miradi mikubwa ikiwemo Julius Nyerere (MW 2,115), Rusumo (MW 80), Kinyerezi I – Extension (MW 185), Malagarasi (MW 45), Kakono (MW 87); na Mtwara (MW 300); ujenzi wa njia za kusafirisha umeme ikiwemo Singida – Arusha – Namanga kV 400, North – West Grid Extension (Mbeya – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma – Nyakanazi) kV 400, Rufiji – Chalinze – Dodoma kV 400, Kinyerezi – Dodoma kV 400, Geita – Nyakanazi kV 220, Rusumo - Nyakanazi kV 220 na Bulyanhulu – Geita kV 220; kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijijini; kuimarisha shughuli za utafiti wa mafuta na gesi asilia na kuhakikisha upatikanaji wa mafuta ya kutosha kupitia utaratibu wa kuagiza mafuta kwa pamoja ili kuendesha shughuli za maendeleo.

**16. Mheshimiwa Spika,** Wizara pia ilizingatia maeneo mengine ambayo ni pamoja na: kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara na Taasisi zake katika kusimamia Sekta ya Nishati; kuboresha mazingira ya ofisi kwa watumishi wa Wizara na Taasisi zake ili kutoa huduma bora zaidi; na kuendelea kuelimisha umma na kuboresha mawasiliano na wadau mbalimbali kuhusu masuala ya nishati.



## **D. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA WIZARA KWA MWAKA 2019/20 NA MPANGO WA BAJETI KWA MWAKA 2020/21**

17. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2020/21, Wizara ya Nishati itaendelea kutekeleza maeneo ya vipaumbele mbalimbali yakiwemo: kuongeza uzalishaji wa umeme nchini kwa kutekeleza mradi mkubwa wa Julius Nyerere (MW 2,115) na miradi mingine ya Kinyerezi I - *Extension* (MW 185), Rusumo MW 80, Ruhudji (MW 358), Rumakali (MW 222) na Malagarasi (MW 45). Aidha, Wizara imeendelea na taratibu za kushirikisha wawekezaji binafsi katika utekelezaji wa miradi ya umeme wa Jua MW 150, umeme wa Upepo MW 200 na Makaa ya Mawe MW 600 kwa njia ya ushindani. Miradi hiyo inatarajiwa kuanza kutekelezwa mwaka 2020/21.

18. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na miradi hiyo ya uzalishaji wa umeme, Serikali pia itaendelea kutekeleza miradi ya kuimarisha mifumo ya usafirishaji wa umeme nchini kwa kutekeleza miradi mbalimbali. Miradi hiyo ni pamoja na: *North - West Grid Extension kV 400*, Singida – Arusha – Namanga **kV 400**, Rufiji - Chalinze – Dodoma **kV 400**, Rusumo – Nyakanazi **kV 220**, Geita – Nyakanazi **kV 220**, Geita – Bulyanhulu **kV 220**, Urambo – Kigoma **kV 132**, Ipole – Katavi **kV 132**, Ibadakuli – Imalilo **132 kV** na Kiteto – Kilindi **132 KV**.

19. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2020/21 maeneo mengine ya kisekta yatakuoziingatiwa na Wizara ni: kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya Tatu ya Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijijini; kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani Tanga nchini Tanzania (*East African Crude Oil Pipeline - EACOP*); kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kusindika Gesi Asilia (LNG); kuimarisha shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia; kuongeza kasi ya usambazaji wa gesi asilia; kuvutia uwekezaji katika sekta ya nishati; na kuendelea kuimarisha utendaji wa Taasisi chini ya Wizara; TANESCO, TGDC, REA, TPDC, PURA na PBPA ili kuongeza ufanisi katika Sekta ya Nishati. Aidha, Serikali itaendelea kuhakikisha uwepo wa mafuta ya kutosha kuendesha shughuli za kiuchumi kupitia Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja.

20. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na maeneo hayo ya kisekta, Wizara pia itazingatia maeneo mengine yanayolenga kuleta tija katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na: kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara na Taasisi zake katika kusimamia Sekta; kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi ili kutoa huduma bora; na kuendelea kuelimisha umma kuhusu masuala ya nishati.

## **SEKTA NDOGO YA UMEME UWEZO WA MITAMBO YA KUZALISHA UMEME**

21. *Mheshimiwa Spika*, uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme iliyounganishwa katika Gridi ya Taifa ni **MW 1,565.72** ambapo **MW 573.70** zinatokana na nguvu ya maji, **MW 892.72** gesi asilia, **MW 88.80** mafuta mazito na dizeli na **MW 10.50** mabaki ya mimea na mazao (*Biomass*). Uwezo wa mitambo hiyo unajumuisha mitambo inayomilikiwa na Serikali kupitia TANESCO ambayo huchangia **asilimia 86.50** na mitambo ya Wazalishaji Binafsi (*IPPs/SPPs*) ambayo huchangia **asilimia 13.50**. Aidha, TANESCO inamiliki mitambo ambayo haijaunganishwa katika Gridi ya Taifa yenye uwezo wa kufua **MW 36.12** na hivyo kufanya jumla ya uwezo wa mitambo ya kufua umeme nchini kufikia **MW 1,601.84**.

22. *Mheshimiwa Spika*, mahitaji ya juu ya umeme katika Gridi ya Taifa yameendelea kuongezeka kutokana na kuongezeka kwa shughuli za uchumi nchini. Tarehe 27 Februari, 2020 mahitaji ya juu ya umeme yalifikia **MW 1,151.66** ikilinganishwa na **MW 1,116.58** zilizofikiwa mwaka 2019. Ongezeko hili ni sawa na **asilimia 3.14**. Aidha, umeme uliozalishwa nchini uliongezeka kutoka **GWh 7,374** mwaka 2018 na kufikia **GWh 7,692** mwaka 2019 sawa na ongezeko la **asilimia 4.3**.

## MIRADI YA KUZALISHA UMEME

### *Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere Hydro Power Project (JNHPP) – MW 2,115*

23. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa **MW 2,115** kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Rufiji. Mkandarasi ambaye ni Kampuni ya *Arab Contractors* yenye ubia na *Elsewedy Electric*, zote za nchini Misri tarehe 15 Juni, 2019 alianza rasmi utekelezaji wa mradi. Katika mwaka 2019/20 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kuanza ujenzi wa bwawa (*main dam*); na kuanza ujenzi wa njia ya kuchepusha maji (*diversion tunnel*). Kwa ujumla utekelezaji wa mradi huu unaendelea vizuri kulingana na Mpango Kazi wake na unatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2022.

24. *Mheshimiwa Spika*, kazi nyingine zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa mgodi wa kuzalisha umeme, njia za kupeleka maji kwenye mitambo, manunuzi ya vifaa mbalimbali vya mradi ambapo shughuli hizo zote zinawiana na Mpango Kazi wake. Gharama za mradi huu ni **Shilingi trilioni 6.55** zinazotokana na fedha za ndani. Mradi huu unamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 Mkandarasi amelipwa **Shilingi trilioni 1.219** sawa na **asilimia 100** ya fedha alizotakiwa kulipwa kwa mujibu wa mkataba.

25. *Mheshimiwa Spika*, jumla ya wafanyakazi wapatao **3,897** wameajiriwa tangu utekelezaji wa mradi uanze ambapo kati ya wafanyakazi hao watanzania ni **3,422** sawa na **asilimia 87.81** na wafanyakazi kutoka nje ya nchi ni **475** sawa na **asilimia 12.19** ya wafanyakazi wote wa mradi. Hadi kukamilika kwa Mradi Watanzania 6,000 wataajiriwa katika shughuli za Mradi.

26. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2020/21, Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi ambapo kazi zitakazofanyika ni pamoja na kuendelea na: ujenzi wa bwawa (*main dam and spillways*); ujenzi wa njia kuu za kupitisha maji (*tunnels*); ujenzi wa eneo la kufunga mitambo ya kufua umeme (*power house*); na ujenzi wa kituo cha kusafirisha umeme (*switch yard*). Jumla ya fedha za ndani **Shilingi trilioni 1.44** zimetengwa katika mwaka 2020/21 kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo.



***Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Rusumo – MW 80***

27. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 80 kwa kutumia maji ya Mto Kagera na unahusisha nchi tatu (3) za Tanzania, Burundi na Rwanda kwa mgawanyo sawa kwa kila nchi. Mradi unagharimu **Dola za Marekani milioni 113** sawa na takriban **Shilingi bilioni 263.87** kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kwa upande wa Tanzania. Hadi sasa, uchimbaji wa eneo la kujenga mitambo (*power house*) umekamilika na ufungaji wa mitambo umefikia **asilimia 52**; kukamilika kwa milango ya kuingiza na kuchepusha maji (*spillway and intake gates*); kukamilika kwa ujenzi wa nyumba za wafanyakazi; na kuendelea na uchimbaji wa handaki la kupitishia maji ambao umefikia **asilimia 56**. Utekelezaji wa mradi kwa ujumla umefikia **asilimia 61**.

28. *Mheshimiwa Spika*, kazi zilizopangwa kufanyika mwaka 2020/21 ni: kuendelea na ufungaji wa mitambo pamoja na ujenzi wa mfumo wa kupitisha maji (*tunnelling system*); ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme; ujenzi wa kituo cha kusafirisha umeme (*switch yard*); na kukamilisha miradi ya kijamii kwa wananchi wanaozunguka eneo la mradi (*Local Area Development Plan – LADP* na *Livelihood Restoration Program – LRP*). Jumla ya **Shilingi milioni 13.846** zimetengwa katika mwaka 2020/21 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi. Mradi huu ulianza mwezi Februari, 2017 na unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Februari, 2021.

***Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Ruhudji – MW 358***

29. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 358 kwa kutumia maji ya Mto Ruhudji na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **kV 400** yenye urefu wa kilomita 170 kutoka Ruhudji hadi katika eneo la Kisada, Iringa kitakapojengwa kituo cha kupoza umeme. Ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme unakadiriwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 407.4** sawa na takriban **Shilingi bilioni 951.34** na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme unakadiriwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 53.2** sawa na takriban **Shilingi bilioni 124.23**. Kazi zilizofanyika mwaka 2019/20 ni pamoja na: uhuishaji wa Upembuzi Yakinifu (*Updating of feasibility study*); usanifu wa awali wa mradi pamoja na uandaaji wa makabrasha ya zabuni ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mradi.

30. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/21 kazi zitakazofanyika ni pamoja na: kukamilisha uhuishaji wa Upembuzi Yakinifu (*Updating of feasibility study*); usanifu wa awali wa Mradi (*Conceptual Design*); na kumpata Mkandarasi wa kujenga mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 255.583** zimetengwa katika mwaka 2020/21 ili kutekeleza kazi hizo. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2021 na kukamilika mwezi Juni, 2024.

***Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Kakono – MW 87***

31. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 87 kwa kutumia maji ya Mto Kagera na njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **kV 220** kutoka Kakono hadi Kyaka yenye urefu wa kilomita 38.5. Katika mwaka 2019/20 kazi zilizokamilika ni pamoja na usanifu wa mradi na uandaaji wa makabrasha ya zabuni. Ujenzi wa mradi huu utagharimu **Dola za Marekani milioni 287.60** sawa na takriban **Shilingi bilioni 671.575**.

32. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2020/21 kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: kulipa fidia wananchi watakaopisha mradi; na kukamilisha Tathmini ya Athari kwa Mazingira. Serikali kupitia TANESCO imetenga **Shilingi bilioni 1.56** kwa ajili ya kulipa fidia. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Desemba, 2021 na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2024.

***Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Rumakali – MW 222***

33. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 222 kwa kutumia maji ya Mto Rumakali katika Mkoa wa Njombe na njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 150 kutoka Rumakali hadi kituo cha kupoza umeme cha Iganjo Mkoani Mbeya. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 388.22** sawa na takriban **Shilingi bilioni 906.53**. Kwa mwaka 2019/20 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: uhuishaji wa Upembuzi Yakinifu (*Updating of feasibility study*); usanifu wa awali wa mradi; na kuandaa makabrasha ya zabuni ya ujenzi wa mradi.

34. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/21 kazi zitakazofanyika ni: kukamilisha kuhuisha Upembuzi Yakinifu na kuanza maandalizi ya ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 23.033** zimetengwa katika mwaka 2020/21 ili kutekeleza kazi hizo. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2021 na kukamilika mwezi Juni, 2024.

***Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Malagarasi– MW 45***

35. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unahusu ujenzi wa kituo cha kuzalisha umeme wa MW 45 kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Malagarasi katika Mkoa wa Kigoma. Aidha, mradi utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **kV 132** yenye urefu wa kilomita 55 kutoka Malagarasi hadi Kidahwe Mkoani Kigoma. Gharama za utekelezaji wa Mradi ni **Dola za Marekani milioni 138.1** sawa na takriban **Shilingi bilioni 322.48**.

36. *Mheshimiwa Spika*, kazi zilizofanyika ni pamoja na: kukamilisha uhuishaji wa Upembuzi Yakinifu wa kituo cha kuzalisha umeme pamoja na uthamini katika kilomita 33 toka kijiji cha Mazungwe hadi Kidahwe.

37. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21 kazi zitakazofanyika ni pamoja na kukamilisha taratibu za kupata fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) na kuanza ujenzi wa mradi. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Septemba, 2020 na kukamilika mwezi Septemba, 2023. Kiasi cha **Shilingi milioni 100** kimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

***Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Kikonge – MW 300***

38. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unahusu ujenzi wa Mtambo wa kuzalisha umeme wa MW 300 kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Ruhuhu katika Mkoa wa Njombe na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 53 kutoka Kikonge hadi kituo cha kupoza umeme cha Madaba. Gharama za utekelezaji wa Mradi zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 750** sawa na takriban **Shilingi trilioni 1.75**.

39. *Mheshimiwa Spika*, kazi zilizotekelezwa katika kipindi cha mwaka 2019/20 ni pamoja na: kukamilika kwa Tathmini ya Mazingira ya Kimkakati (*Strategic Environmental & Social Assessment – SESA*); na kuendelea na Upembuzi Yakinifu (*Feasibility Study*).



40. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/21 kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: kukamilisha Upembuzi Yakinifu (*Feasibility Study*); na kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii; pamoja na kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mradi. Kiasi cha **Shilingi bilioni 1.038** zimetengwa katika mwaka 2020/21 ili kutekeleza kazi hizo. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Novemba, 2021 na kukamilika mwezi Desemba, 2023.

*Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Kinyerezi I Extension – MW 185*

41. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unahusu upanuzi wa kituo cha Kinyerezi I – MW 150 kwa kuongeza mitambo itakayozalisha **MW 185** na hivyo kufanya kituo hicho kuzalisha jumla ya **MW 335**. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa **asilimia 100** kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 188** sawa na takriban **Shilingi bilioni 439.1**. Kwa ujumla ujenzi wa mradi umefikia **asilimia 84**.

42. *Mheshimiwa Spika*, Kutokana na mkandarasi wa awali kushindwa kukamilisha mradi huu, Serikali kupitia TANESCO inakamilisha taratibu za kumpata mkandarasi wa kukamilisha kazi zilizobaki. Fedha za ndani **Shilingi bilioni 138.0** zimetengwa katika mwaka 2020/21 kwa ajili ya kukamilisha mradi huu. Ujenzi wa mradi huu unatarajia kukamilika mwezi Desemba, 2020.

*Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Mtwara – MW 300*

43. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unahusu ujenzi wa mitambo ya kuzalisha umeme wa **MW 300** kwa kutumia gesi asilia katika Mkoa wa Mtwara. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa **Dola za Marekani milioni 421.1** sawa na takriban **Shilingi bilioni 983.31**. Mradi utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** yenye urefu wa kilomita 270 kutoka Mtwara hadi Somanga Fungu kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 113** sawa na takriban **Shilingi bilioni 263.87** na vituo vya kupoza umeme ambavyo vitagharimu **Dola za Marekani milioni 166.2** sawa na takriban **Shilingi bilioni 388.09**. Katika mwaka 2019/20 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kukamilika kwa Upembuzi Yakinifu wa kituo cha kuzalisha umeme na njia ya kusafirisha umeme; na Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii katika miundombinu wezeshi (maji, barabara na bomba la gesi).

44. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/21 kazi zitakazofanyika ni kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi na kukamilisha taratibu za upatikanaji wa fedha za ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme. Serikali imetenga **Shilingi milioni 500** kuwezesha utekelezaji wa kazi hizo. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2021 na kukamilika mwezi Septemba 2024.

*Miradi wa Kuzalisha Umeme ya Nishati Jadidifu (Umeme Jua MW 150, Upepo MW 200) na Makaa ya Mawe MW 600*

45. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/20 Serikali imeendelea na taratibu za kuwapata Wazalishaji Binafsi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hii. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 tathmini ya zabuni (*tender evaluation*) kwa kampuni 11 zilizorudisha zabuni kati ya 38 zilizopita mchujo wa kwanza (*Shortlisted*) ilikamilika. Kazi inayoendelea sasa ni kukamilisha maandalizi kwa ajili ya kuanza majadiliano na kampuni hizo.

46. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha mwaka 2020/21, Serikali itakamilisha taratibu za kuwapata Wawekezaji Binafsi wenye gharama na masharti nafuu katika kutekeleza miradi

hiyo. Utekelezaji huo unatarajiwa kuanza mwezi Novemba, 2020 na kukamilika mwezi Oktoba, 2022.

## MIRADI YA KUSAFIRISHA UMEME

### *Mradi wa Kusafirisha umeme kutoka Singida – Arusha – Namanga kV 400*

47. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya umeme msongo wa **kV 400** yenye urefu wa kilomita 414 kutoka Singida hadi Namanga kupitia Arusha. Aidha, mradi unahusisha ujenzi wa kituo kipya cha kupoza umeme cha Kisongo Mkoani Arusha na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Singida. Kazi nyingine ni usambazaji wa umeme katika vijiji 19 vilivyo jirani na mkuza wa njia ya umeme katika Mikoa ya Singida, Manyara na Arusha. Gharama za mradi ni **Dola za Marekani milioni 258.82** sawa na takriban **Shilingi bilioni 604.37**. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 jumla ya nguzo 621 kati ya 1,072 zimesimikwa na hivyo kufanya utekelezaji wa mradi kufikia **asilimia 67**.

48. *Mheshimiwa Spika*, utekelezaji wa mradi huu unaenda sambamba na utekelezaji wa mradi wa *Backbone* awamu ya pili (*Backbone Phase II*) unaolenga kuongeza uwezo (*Upgrade*) wa vituo vya kupoza umeme kutoka **kV 220** mpaka **kV 400** katika Mikoa ya Iringa, Shinyanga, Singida na Dodoma ambapo utekelezaji umefikia **asilimia 83**.

49. *Mheshimiwa Spika*, kazi zilizopangwa kufanyika mwaka 2020/21 ni: kuendelea na ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na vituo vya kupoza umeme vya Dodoma na Singida. Jumla ya **Shilingi bilioni 30.21** fedha za nje zimetengwa katika mwaka 2020/21 ili kutekeleza kazi hizo. Mradi huu ulianza kutekelezwa mwezi Machi, 2018 na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Desemba, 2020.

### *Mradi wa njia ya kusafirisha Umeme kutoka Makambako hadi Songea kV 220 na Usambazaji wa Umeme Vijijini kwa Mikoa ya Njombe na Ruvuma*

50. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **kV 220**, yenye urefu wa kilomita 250 kutoka Makambako hadi Songea kupitia Madaba pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Madaba na Songea na upanuzi wa kituo cha Makambako. Mradi huu umekamilika kwa **asilimia 100** mwezi Septemba, 2018 na kazi ya kuunganisha wateja wapya inaendelea.

51. *Mheshimiwa Spika*, Vilevile, kazi ya kufunga *reactor* na *distribution panel* katika kituo cha Madaba ilikamilika mwezi Septemba, 2019 na kwa sasa hali ya upatikanaji umeme katika Mkoa wa Ruvuma imeimarika. Serikali kupitia TANESCO na REA inaendelea kuwahamasisha wananchi wajitokeze kwa wingi kuunganishiwa umeme.

### *Mradi wa Njia ya kusafirisha Umeme kutoka Bulyanhulu – Geita kV 220*

52. *Mheshimiwa Spika*, Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 55 kutoka Bulyanhulu hadi Geita na kituo cha kupoza umeme cha Geita, upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Bulyanhulu, usambazaji wa umeme katika Vijiji 10 vilivyopo katika eneo la mradi na kuunganisha wateja wa awali 1,500 katika Mkoa wa Geita. Gharama za mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 23.0** sawa na takriban **Shilingi bilioni 53.71**. Kazi ya ujenzi na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme na ujenzi wa njia za kusafirisha umeme zimekamilika kwa **asilimia 82**. Mkandarasi wa usambazaji



umeme vijijini anaendelea na kazi za ufungaji wa mashineumba na kuunganishia wateja. Kazi ya usambazaji umeme imefikia **asilimia 92** na hivyo kufanya utekelezaji mzima wa mradi kufikia **asilimia 85**. Ujenzi wa mradi huu ulianza mwezi Januari, 2019 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2020. Aidha, kwa mwaka 2020/21 Serikali itaendelea kufuatilia na kutathmini ubora wa kazi zilizotekelezwa.

***Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kutoka Geita – Nyakanazi kV 220***

**53. Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 144, ujenzi wa vituo vya kupoza umeme Geita na Nyakanazi na kusambaza umeme katika vijiji 32 vinavyopitiwa na mradi katika maeneo ya Geita Mjini hadi Bwanga na Nyakanazi hadi Kakonko. Gharama za utekelezaji wa Mradi huu ni **EURO milioni 45** sawa na takriban **Shilingi bilioni 117.79**. Katika mwaka 2019/20 kazi zilizofanyika ni pamoja na: upimaji wa udongo na usanifu wa mradi; ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; na kuanza ujenzi wa kituo cha kupoza umeme.

**54. Mheshimiwa Spika**, kazi zilizopangwa kutekelezwa mwaka 2020/21 ni pamoja na: kukamilisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme kutoka Geita hadi Nyakanazi; kukamilisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Nyakanazi na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Geita; na kusambaza umeme katika vijiji 32 vitakavyopitiwa na mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 25.33** zimetengwa katika mwaka 2020/21 kwa ajili ya shughuli za mradi huu. Ujenzi wa mradi huu ulianza mwezi Agosti, 2019 na unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2021.

***Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kutoka Rusumo – Nyakanazi kV 220***

**55. Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 98 kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha Rusumo hadi Nyakanazi. Gharama za Mradi ni **Dola za Marekani milioni 35** sawa na takriban **Shilingi bilioni 81.73**. Katika mwaka 2019/20 kazi zilizofanyika ni pamoja na: upimaji wa njia (*detail survey*); kusafisha njia ya umeme na ujenzi wa barabara za kuwezesha kufikia eneo la mradi (*access roads*); na usanifu wa nguzo (*Tower Spotting*). Ujenzi wa mradi huu ulianza mwezi Oktoba, 2019 na unatarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2020.

***Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kutoka Iringa - Mbeya – Tunduma - Sumbawanga – Mpanda - Kigoma – Nyakanazi (North West Grid) kV 400***

**56. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** kutoka Iringa – Mbeya – Tunduma – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma – Nyakanazi yenye urefu wa kilomita 1,384. Mradi utatekelezwa kwa awamu tatu kama ifuatavyo:

***Awamu ya Kwanza: Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kutoka Iringa – Mbeya – Tunduma hadi Sumbawanga kV 400***

**57. Mheshimiwa Spika**, awamu hii inahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** kutoka Iringa kupitia Mbeya, Tunduma hadi Sumbawanga yenye urefu wa kilomita 624 na vituo vya kupoza umeme vya Kisada, Mbeya, Tunduma na Sumbawanga.

Awamu hii itagharimu jumla ya **Dola za Marekani milioni 465** sawa na takriban **Shilingi trilioni 1.085**. Kazi zilizotekelezwa kwa mwaka 2019/20 ni pamoja na: kudurusu taarifa ya awali ya Upembuzi Yakinifu kati ya Mbeya na Sumbawanga; kukamilisha uthamini wa mali zitakazopitiwa na mradi na uainishaji wa mipaka ya mkuza wa mradi.

**58. Mheshimiwa Spika**, kazi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka 2020/21 ni: ulipaji wa fidia wananchi watakaopisha mradi; kuhuisha Tathmini ya Athari kwa Mazingira; kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mradi; na kuanza ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na vituo vinne (Kisada, Mbeya, Tunduma na Sumbawanga) vya kupoza umeme. Jumla ya **Shilingi bilioni 1** zimetengwa katika mwaka 2020/21 ili kutekeleza kazi hizo. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Septemba, 2020 na kukamilika mwezi Novemba, 2022.

***Awamu ya Pili: Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kutoka Nyakanazi hadi Kigoma kV 400***

**59. Mheshimiwa Spika**, awamu hii itahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** kutoka Nyakanazi hadi Kigoma yenye urefu wa kilomita 280, ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Kidahwe Mkoani Kigoma, upanuzi wa kituo cha kupoza umeme Nyakanazi na usambazaji wa umeme vijijini. Gharama ya Mradi huu ni **Dola za Marekani milioni 187** sawa na takriban **Shilingi bilioni 433.17**. Kazi zilizofanyika kwa mwaka 2019/20 ni pamoja na: kuendelea na kazi ya Upembuzi Yakinifu na uandaaji wa nyaraka za kumpata Mkandarasi wa ujenzi; kukamilisha ununuzi wa vifaa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kuwaunganishia umeme wateja 5,000 katika Mkoa wa Kigoma; na kukamilika kwa tathmini na kuanza kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa mradi katika kituo cha kupoza umeme cha Kidahwe.

**60. Mheshimiwa Spika**, kazi zilizopangwa kutekelezwa mwaka 2020/21 ni pamoja na: kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; kukamilisha Upembuzi Yakinifu; na kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 34.28** zimetengwa ili kutekeleza kazi hizo. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2020 na kukamilika mwezi Juni, 2022.

***Awamu ya Tatu: Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kutoka Sumbawanga – Mpanda – Kigoma kV 400***

**61. Mheshimiwa Spika**, awamu hii inahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** kutoka Sumbawanga hadi Kigoma kupitia Mpanda yenye urefu wa kilometa 480. Mradi huu unakadiriwa kugharimu **Dola za Marekani milioni 200** sawa na takriban **Shilingi bilioni 463**. Kwa sasa Mradi upo katika hatua ya kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kuandaa ripoti ya mazingira. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2022 na kukamilika mwezi Juni, 2024.

***Mradi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kutoka Kituo cha Kuzalisha Umeme Cha Julius Nyerere kV 400***



62. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha Julius Nyerere hadi Dodoma kupitia Chalinze na Chalinze hadi Kinyerezi. Mradi utatekelezwa kwa awamu mbili kama ifuatavyo:

*Awamu ya Kwanza: Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kutoka Kituo cha Kuzalisha Umeme cha Julius Nyerere – Chalinze – Dodoma kV 400*

63. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa **kV 400** wenye urefu wa kilomita 505 kutoka kituo cha kuzalisha umeme cha Julius Nyerere kupitia Chalinze mkoani Pwani hadi Dodoma na upanuzi wa vituo vya kupoza umeme vya Chalinze na Dodoma. Gharama za mradi ni **Dola za Marekani milioni 305.21** sawa na takriban **Shilingi bilioni 712.71**. Kazi zilizofanyika mwaka 2019/20 ni kukamilika kwa Upembuzi Yakinifu, uandaaji wa makabrasha ya zabuni na tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi.

64. *Mheshimiwa Spika*, kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2020/21 ni: kulipa fidia wananchi watakaopisha mradi; kumpata Mkandarasi wa ujenzi; na kuanza ujenzi wa mradi. **Shilingi bilioni 8.14** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2020 na kukamilika mwezi Desemba, 2021.

*Awamu ya Pili: Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kutoka Chalinze hadi Kinyerezi kV 400*

65. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 400** yenye urefu wa kilomita 115 kutoka Chalinze hadi Kinyerezi pamoja na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kinyerezi. Gharama za mradi ni **Dola za Marekani milioni 112** sawa na takriban **Shilingi bilioni 261.53**. Kazi zilizotekelezwa kwa mwaka 2019/20 ni kukamilisha Upembuzi Yakinifu; na tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi.

66. *Mheshimiwa Spika*, kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2020/21 ni pamoja na: kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme na upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha Kinyerezi; kuanza kulipa fidia wananchi watakaopisha mradi; na kuanza ujenzi wa mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 3.89** zimetengwa katika mwaka 2020/21 kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Agosti, 2020 na kukamilika mwezi Desemba, 2021.

*Mradi wa kuunganisha Mikoa ya Kigoma na Katavi katika Gridi ya Taifa*

67. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 132** kwa ajili ya kuunganisha mikoa ya Kigoma na Katavi katika Gridi ya Taifa. Mradi huu ulizinduliwa na Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 11 Oktoba, 2019. Mradi huu unatekelezwa katika awamu mbili kama ifuatavyo:

(i) *Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kwa Ajili ya Kuunganisha Mkoa wa Kigoma katika Gridi ya Taifa kutokea Tabora kV 132*

68. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 132** kutoka Tabora hadi Kigoma kupitia Urambo na Nguruka umbali wa kilomita 395 pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Urambo, Nguruka na Kidahwe. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa takriban **Shilingi bilioni 66.7**.

69. *Mheshimiwa Spika*, kazi zilizotekelezwa mwaka 2019/20 ni pamoja na kukamilisha: Upembuzi Yakinifu; upatikanaji wa maeneo ya kujenga vituo vya kupoza umeme vya Urambo, Nguruka na Kidahwe; upimaji wa njia ya kusafirisha umeme (*route survey*); na uwekaji wa alama za mipaka ya njia (*route demarcation*) ya kusafirisha umeme pamoja na ujenzi wa kituo cha kupoza umeme cha Urambo.

70. *Mheshimiwa Spika*, kazi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka 2020/21 ni: kuendelea na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme; kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; na kuanza ujenzi wa njia za kusafirisha umeme kwenda Kigoma kutoka Tabora. **Shilingi bilioni 5** zimetengwa ili kutekeleza kazi hizo. Kazi za ujenzi wa Mradi zilianza mwezi Oktoba, 2019 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2021.

(ii) *Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kwa Ajili ya Kuunganisha Mkoa wa Katavi katika Gridi ya Taifa Kutoka Tabora kV 132*

71. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 132** kutoka Tabora hadi Katavi kupitia Ipole na Inyonga umbali wa kilomita 381 pamoja na ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Ipole, Inyonga na Mpanda mkoani Katavi. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa **Shilingi bilioni 64.5**.

72. *Mheshimiwa Spika*, kazi zilizofanyika mwaka 2019/20 ni pamoja na kukamilisha: Upembuzi Yakinifu wa awali (*Pre-feasibility Study*); upatikanaji wa maeneo ya kujenga vituo vya kupoza umeme vya Ipole, Inyonga na Mpanda; na uwekaji wa alama za mipaka (*route demarcation*) ya njia ya kusafirisha umeme. Aidha, tathmini ya mali za wananchi watakaopisha ujenzi wa mradi na Tathmini ya Athari kwa Mazingira zinaendelea. Ujenzi wa kituo cha Mpanda ulianza mwezi Septemba 2019 na kituo cha Inyonga umeanza mwezi Aprili 2020.

73. *Mheshimiwa Spika*, kazi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka 2020/21 ni: kukamilisha ujenzi wa vituo vya kupoza umeme; kulipa fidia wananchi watakaopisha mradi; na kuanza ujenzi wa njia za kusafirisha umeme kwenda Kigoma kutokea Tabora. **Shilingi bilioni 5** zimetengwa ili kutekeleza kazi hizo. Mradi ulianza mwezi Januari, 2019 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2021.

*Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kV 220 na Kituo cha Kupoza Umeme katika Mkoa wa Simiyu*

74. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 160 kutoka Ibadakuli Mkoani Shinyanga hadi Imalilo Mkoani Simiyu. Gharama ya mradi inakadiriwa kuwa **Shilingi bilioni 75**. Hadi sasa, ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa kituo cha kupoza umeme Imalilo umekamilika.



75. *Mheshimiwa Spika*, kazi zilizopangwa kufanyika kwa mwaka 2020/21 ni pamoja na kukamilisha: Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii; uainishaji wa mipaka ya mkuza wa njia ya kusafirisha umeme; na tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi. Katika mwaka 2020/21, Serikali kupitia TANESCO imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 1** kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2021 na kukamilika mwezi Desemba, 2022.

*Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Mwendo Kasi (Standard Gauge Railway – SGR) Awamu ya Kwanza (Lot I) kV 220*

76. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilomita 160 kutoka Kinyerezi - Dar es Salaam hadi Msamvu - Morogoro kwa ajili ya kuendesha Treni ya Mwendokasi (*Standard Gauge Railway – SGR*) awamu ya kwanza. Gharama ya mradi ni **Shilingi bilioni 76.23** na unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa asilimia 100.

77. *Mheshimiwa Spika*, kazi zilizofanyika ni pamoja na: ujenzi wa misingi ya minara ya umeme (*Tower Foundations*) 444 kati ya 456 imejengwa; ujenzi wa minara (*Towers erections*) 404 kati ya 456; uvutaji wa nyaya kwa urefu wa kilomita 88 kati ya 160 na kulipa fidia wananchi waliopisha mradi. Utekelezaji wa mradi huu kwa ujumla umefikia **asilimia 89**. Mradi ulianza kutekelezwa mwezi Januari, 2019, na unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Mei, 2020.

*Ujenzi wa Njia ya Kusafirisha Umeme kwa Ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Mwendo Kasi (Standard Gauge Railway – SGR) Awamu ya Pili (Lot II) kV 220*

78. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unahusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** yenye urefu wa kilometa 410 kutoka Msamvu, mkoani Morogoro hadi Makutupora, mkoani Singida kwa ajili ya kuendesha treni ya mwendokasi. Mradi huu umegawanyika katika sehemu kuu mbili (2) ambapo sehemu ya kwanza ni kutoka Morogoro hadi Ihumwa - Dodoma, yenye urefu wa kilomita 236 na sehemu ya pili ya mradi huu ni kutoka Ihumwa hadi Kintinku - Singida wenye urefu wa kilomita 174. Kazi za ujenzi wa mradi huu zinatarajiwa kuanza mwishoni mwa mwezi Mei, 2020 na kukamilika mwezi Julai 2021. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa **Shilingi bilioni 201**.

## MIRADI YA KUBORESHA NJIA ZA USAMBAZAJI UMEME

*Mradi wa Kuboresha Mfumo wa Usambazaji Umeme Katika Jiji la Dodoma*

79. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu utahusisha ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa **kV 220** kutoka Zuzu kwenda Msalato na kutoka Zuzu kwenda Kikombo pamoja na ujenzi wa vituo viwili (2) vipya vya kupoza na kusambaza umeme katika maeneo ya Msalato na Ihumwa Jijini Dodoma. Gharama ya mradi ni **Dola za Marekani milioni 167.7** sawa na takriban **Shilingi bilioni 388.46**. Kazi zilizofanyika kwa mwaka 2019/20 ni pamoja na kukamilisha Upembuzi Yakinifu wa njia ya kusafirisha umeme msongo wa **kV 220** na njia za kusambaza umeme msongo wa **kV 33**. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2021 baada ya kukamilika taratibu za kupata ufadhili na wakandarasi

wa kutekeleza mradi. Mradi unategemewa kukamilika mwezi Julai, 2023.

*Mradi wa Usambazaji Umeme kwa Maeneo ya Mijini (Urban Electrification Program)*

**80. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unalenga kuwezesha TANESCO kuongeza kasi ya kuunganisha wateja maeneo ya mijini na kupanua miundombinu ya usambazaji umeme ili kuhamasisha ujenzi wa viwanda. Katika mwaka 2019/20, kazi zilizofanyika ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa njia za usambazaji umeme katika maeneo mbalimbali nchini ambapo jumla ya kilomita 312 za msongo wa **kV 33** na kilomita 578 msongo wa **kV 0.4** zimejengwa. Aidha, mashineumba 216 zimefungwa na wateja wapya 9,071 wameunganishwa.

**81. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2020/21, kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na kujenga jumla ya kilomita 280.16 za njia ya msongo wa **kV 11**, kilomita 734.8 za msongo wa **kV 33**, kilomita 4,126.74 za msongo wa **kV 0.4**, kufunga mashineumba 1,161, kuunganisha wateja wapya 149,098 na maboresho ya miundombinu ya usambazaji. Jumla ya **Shilingi bilioni 209.8** zimetengwa katika mwaka 2020/21 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo. Utekelezaji wa mradi huu ni endelevu katika mikoa yote.

## MIRADI YA KUSAMBAZA UMEME VIJIJINI

**82. Mheshimiwa Spika**, mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu unalenga kufikisha umeme katika vijiji 7,873. Aidha, hadi kufikia Desemba 2015, jumla ya vijiji 2,018 vilikuwa vimefikwa na huduma ya umeme. Idadi hiyo imeongezeka na kufikia 9,112 mwezi Aprili, 2020 sawa na ongezeko la vijiji 7,094.

**83. Mheshimiwa Spika**, Vijiji 1,822 ambavyo ni sawa na asilimia 14.86 vitakavyobakia baada ya mwezi Juni, 2020 vitapelekwa umeme kupitia Mradi wa Kupeleka Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili (*Turnkey Phase III – Round II*) uliopangwa kutekelezwa katika Mwaka 2020/21. Kukamilika kwa mradi huo kutafanya vijiji vyote kufikiwa na umeme.

**84. Mheshimiwa Spika**, kazi zitakazofanyika mwaka 2020/21 ni pamoja na: kujenga miundombinu ya kusambaza umeme; kuendelea kusambaza umeme katika maeneo yaliyopo pembezoni mwa Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani; kusambaza umeme kwenye vitongoji vilivyopitiwa na miundombinu ya usambazaji umeme wa msongo wa kati kupitia Mradi wa ujazilizi (*Densification*); kuunganisha wateja na ufungaji wa mifumo ya nishati jadidifu katika maeneo yaliyo mbali na Gridi zikiwemo Taasisi za Umma, visiwa katika Bahari ya Hindi, Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na Delta ya Rufiji.

**85. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 jumla ya Wilaya na Halmashauri 36 za Tanzania Bara vijiji vyake vyote vimefikwa na ujenzi wa miundombinu ya umeme. Vitongoji na maeneo ambayo hayajafikiwa na miundombinu ya umeme yataendelea kupelekwa umeme kuanzia mwezi Juni, 2020.

**86. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwezi Januari, 2016 hadi Machi 2020, jumla ya Taasisi **11,164** zimeunganishwa umeme ikilinganishwa na Taasisi **4,036** zilizokuwa



zimeunganishiwa kufikia mwezi Desemba, 2015 sawa na ongezeko la **asilimia 184.88**. Ongezeko hilo linafanya jumla ya Taasisi zilizounganishiwa umeme kufikia **15,200**.

### **Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu - Mzunguko wa Kwanza**

**87. Mheshimiwa Spika**, lengo la mradi huu ni kufikisha umeme katika vijiji 3,559 ambavyo havijafikiwa na umeme. Gharama za mradi ni **Shilingi trilioni 1.157**. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020 jumla ya vijiji 2,659 sawa na **asilimia 70.21** vimepatiwa umeme na kuunganisha jumla ya wateja 75,210 kati ya 180,768 waliolengwa. Mradi ulianza mwezi Julai, 2018 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2020. Katika mwaka 2020/21, Serikali itaendelea kusimamia na kutathmini ufanisi wa mradi.

### **Miradi ya Usambazaji Umeme katika Maeneo ambayo yamefikwa na Miundombinu ya Umeme (*Densification*)**

#### **(i) Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa Pili A**

**88. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unalenga kupeleka umeme kwenye vitongoji ambavyo havijapatiwa umeme katika mikoa tisa (9) ya Dodoma, Kilimanjaro, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Singida, Pwani, Tanga, na Mbeya ambapo jumla ya vitongoji 1,103 na wateja wa awali 69,079 wataunganishiwa umeme. Mradi huu utagharimu **Shilingi bilioni 197.8**. Utekelezaji wa mradi huu umeanza mwezi Mei, 2020 na unatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2021.

#### **(ii) Mradi wa Ujazilizi Mzunguko wa Pili B**

**89. Mheshimiwa Spika**, mradi huu utahusisha kupeleka umeme katika vitongoji ambavyo havijafikiwa na umeme katika mikoa 16 ya Kagera, Geita, Mara, Simiyu, Kigoma, Katavi, Rukwa, Iringa, Njombe, Morogoro, Ruvuma, Mtwara, Lindi, Manyara, Arusha na Songwe ambapo jumla ya vitongoji 2,400 vitapatiwa umeme na kuunganishwa wateja wa awali 95,000 kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 100**. Mradi huu unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2020 na kukamilika mwezi Mei, 2021.

### **Mradi wa Usambazaji Umeme katika Vijiji vilivyopo Pembezoni mwa Miji (vijiji miji) – Peri Urban**

**90. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusisha kusambaza umeme katika maeneo yaliyopo pembezoni mwa miji (vijiji miji) katika wilaya za Mkoa wa Pwani na Wilaya ya Kigamboni ambapo ulianza kutekelezwa mwezi Agosti, 2019 katika mitaa 50, vijiji 36, vitongoji 76 na maeneo 88. Mradi unahusisha ujenzi wa njia za msongo wa kati za urefu wa kilomita 623.65, msongo mdogo kilomita 1,277.8, ufungaji wa mashineumba 442 na kuunganisha wateja wa awali 37,713 kwa gharama ya **Shilingi bilioni 74.33**. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2020 ambapo jumla ya vijiji, vitongoji na mitaa 218 vinatarajiwa kuunganishiwa umeme. Aidha, katika Mwaka 2020/21, Serikali imepanga kutekeleza mradi wa kusambaza umeme katika maeneo yaliyopo pembezoni mwa Jiji la Dodoma na Mwanza. Jumla ya **Shilingi bilioni 29** zimetengwa kutekeleza mradi huo.

### Miradi ya Uendelezaji wa Nishati Jadidifu - *Off-Grid*

91. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unahusu usambazaji wa nishati jadidifu katika maeneo yaliyo nje ya mfumo wa gridi ya Taifa pamoja na visiwa. Katika Awamu ya Kwanza, jumla ya Kampuni Binafsi 14 zimepatiwaniwa **Shilingi bilioni 16.88** na hivyo kuwezesha vijiji 102 kati ya 119 vilivyopo kwenye Mpango kupatiwa umeme ambayo ni sawa na **asilimia 86**. Vijiji vilivyobaki 57 kati ya vijiji vyote 176 vitapatiwa umeme kupitia Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili uliopangwa kutekelezwa katika mwaka 2020/21.

92. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2019/20 Wizara ilitangaza zabuni za kuwapata waendelezaji wa miradi ya nishati jadidifu nje ya mfumo wa Gridi ya Taifa (*Call for Proposal – Round 2*) mwezi Novemba, 2019 ambapo maandiko ya miradi (*Project proposals*) kutoka Kampuni 18 yenye thamani ya **Shilingi bilioni 36** yamepokelewa. Hatua inayofuata ni waombaji waliokidhi vigezo kuwasilisha taarifa kamili za mradi na mpango biashara kwa ajili ya uhakiki na kuanza utekelezaji.

### Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu - Mzunguko wa Pili

93. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu utahusisha kusambaza umeme katika vijiji 1,822 vilivyobaki. Kazi za mradi zitahusisha ujenzi wa kilometa 35,581 za njia za umeme za msongo wa kati (kV 33), ujenzi wa kilometa 21,777 za msongo mdogo (kV 0.4), kufunga mashineumba 7,386 na kuunganisha wateja wa awali zaidi ya 582,937. Ujenzi wa mradi utanza mwezi Julai, 2020 na kukamilika mwezi Juni, 2021. Katika mwaka wa fedha wa 2020/21 jumla ya **Shilingi bilioni 297.43** zimetengwa kugharamia utekelezaji wa mradi huo.

## SEKTA NDOGO YA NISHATI JADIDIFU

### Uzalishaji Umeme Kutumia Vyanzo vya Nishati Jadidifu

94. *Mheshimiwa Spika*, nishati jadidifu ni mojawapo ya vyanzo vya nishati ambavyo vimejengewa mazingira wezeshi ili kuchangia upatikanaji wa nishati nchini. Katika mwaka 2019/20, Wizara kwa kushirikiana na EWURA na TANESCO imekamilisha durusu za Kanuni za uendelezaji miradi midogo ya umeme kupitia wazalishaji wadogo *Electricity (Development of Small Power Projects) Rules, 2019*. Kutokana na Kanuni hizo, kuanzia mwezi Juni 2019, Serikali kupitia EWURA imeanza kudhibiti bei zinazotowwa na makampuni yanayotoa huduma za umeme katika maeneo ambayo hayajafikiwa na Gridi ya Taifa ili kuweka ulinganifu wa bei za umeme kwa watumiaji.

95. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/20 Serikali kupitia EWURA imesajili miradi 12 midogo ya uzalishaji na usambazaji umeme nchini yenye uwezo wa **kW 317.78** kwa kutumia nguvu ya jua. Miradi hiyo inaendeshwa na Kampuni za PowerCorner (T) Ltd na PowerGen Renewable Energy Ltd katika Kijiji cha Kiegei Wilaya ya Nachingwea; Kijiji cha Lukumbule, Wilaya ya Tunduru; Kijiji cha Holola, Wilaya ya Nanyumbu; Kijiji cha Kalya,



Wilaya ya Uvinza; Kijiji cha Kagerankanda, Wilaya ya Kasulu; Kijiji cha Itabagumba, Wilaya ya Buchosa; katika vijiji vya Busenge, Kanyala, Iglansoni, Mwenge na Mgambo, Wilaya ya Sikonge. Vilevile, EWURA imetoa leseni za kipindi kifupi kwa Kampuni ya Mwenga Hydro Ltd kwa mradi wa kuzalisha umeme MW 2.5 kwa kutumia nguvu za maji. Umeme huu utaingizwa katika Gridi ya Taifa na kuuzwa kwa wananchi wa Vijiji vya jirani.

### **Matumizi Bora ya Nishati (*Energy Efficiency*)**

**96. Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Matumizi Bora ya Nishati unalenga kutoa mwongozo wa utekelezaji wa masuala ya matumizi sahihi ya nishati katika sekta za ujenzi, usafiri, umeme na nishati kwa matumizi ya nyumbani ikiwemo kupikia. Katika mwaka 2019/20, Wizara imeshiriki katika maandalizi ya mradi wa kikanda wa *Energy Efficient Lighting and Appliances* (EELA).

**97. Mheshimiwa Spika**, kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka 2020/21 ni pamoja na: kuhuisha Mkakati wa Kitaifa wa Matumizi Bora ya Nishati (*National Energy Efficiency Strategy*) katika Mpango Kazi wa Matumizi Bora ya Nishati; kuzijengea uwezo wa kitaalamu na vifaa taasisi zitakazoshiriki katika utekelezaji wa Mpango Kazi wa Matumizi Bora ya Nishati; na kuanzisha miradi ya Mfano kwa nia ya kuhamasisha matumizi bora ya nishati nchini.

### **Programu ya Nishati Endelevu kwa Wote (*Sustainable Energy for All – SE4ALL*)**

**98. Mheshimiwa Spika**, programu hii inafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa-UNDP. Kupitia programu hii, mwaka 2018 Wizara kwa kushirikiana na TANESCO ilihakiki na kubainisha maeneo yanayofaa kwa uzalishaji wa nishati ya umeme-jua katika maeneo ya Same (Kilimanjaro), Zuzu (Dodoma) na Manyoni (Singida). Mwaka 2019 ulifanyika Upembuzi Yakinifu wa Awali (*Pre-feasibility Study*) katika eneo la Mkwese, Manyoni na kubaini uwezekano wa kuzalisha MW 150 za umeme Jua. Kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka 2020/21 ni kukamilisha Upembuzi Yakinifu katika eneo la Mkwese na kuanza hatua za awali za utekelezaji wa mradi. Jumla ya **Shilingi milioni 460** zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

### **Kuridhia na Kutekeleza Mikataba ya Kimataifa Katika Uendelezaji wa Nishati Jadidifu**

**99. Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za uendelezaji wa nishati jadidifu hapa nchini, mwaka 2019 Serikali kupitia Wizara ya Nishati ilikamilisha taratibu za kujiunga na Ushirikiano wa Kimataifa wa Nishati ya Jua (*International Solar Alliance – ISA*). Kupitia Bunge lako Tukufu, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliridhia Mkataba huo mwezi Novemba, 2019. Kujiunga na Taasisi hiyo kutainufaisha Tanzania katika kupata misaada, mikopo nafuu, teknolojia pamoja na utaalam katika uendelezaji wa miradi ya nishati ya jua.

### **Uendelezaji wa Rasilimali ya Jotoardhi (*Geothermal*)**

**100. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Kampuni Tanzu ya TANESCO (TGDC), katika mwaka 2019/20 imeendelea na utekelezaji wa miradi mitano (5) ya kimkakati ya jotoardhi ambayo ni Ngozi, Kiejo-Mbaka, Songwe, Luhoi na Natron. Sambamba na utekelezaji wa miradi hiyo, Serikali imeendelea kuweka mazigira wezeshi ikiwemo kuandaa Sheria mahsusi kwa ajili ya kusimamia na kuendeleza jotoardhi nchini. Maandalizi ya Sheria hiyo yamefikia hatua nzuri ambapo wadau husika wametoa maoni. Aidha, kukamilika kwa Sheria hiyo kutaimairisha mfumo wa kitaasisi katika uendelezaji, usimamizi na udhibiti wa rasilimali ya jotoardhi nchini. Kwa mwaka 2019/20, Serikali kupitia TGDC imeendelea na utekelezaji wa miradi mitatu (3) ya kipaumbele ambayo ni Ngozi, Songwe na Kiejo-Mbaka kama ifuatavyo:

*(i). Mradi wa Ngozi (Mbeya)*

**101. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusisha uzalishaji umeme wa **MW 30** katika chanzo cha mlima wa volkano wa Ngozi. Kwa mwaka 2019/20 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kuandaa Mpango Kazi wa uchorongaji na kusimamia uchorongaji; usanifu wa visima; uainishaji wa vigezo vya mitambo kwa ajili ya uchorongaji; kununua mtambo wa uchorongaji wa visima; kubainisha njia ya miundombinu ya barabara na maji pamoja na kukamilisha usanifu wa awali wa miundombinu.

**102. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21, Serikali kupitia TGDC itakamilisha shughuli za uchorongaji wa visima vitatu (3) vya utafiti kwa ajili ya uhakiki wa rasilimali ya jotoardhi katika maeneo hayo. Jumla ya **Shilingi milioni 419** zimetengewa kwa ajili ya kazi hizo.

*(ii). Mradi wa Songwe*

**103. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusu uzalishaji wa umeme wa **MW 5** na matumizi mengineyo (*direct heat uses*) katika eneo la Majimoto-Songwe. Kazi zilizofanyika ni pamoja na: upatikanaji wa leseni ya eneo la Songwe; kusanifu mradi wa matumizi mengine pamoja na kutwaa ardhi kwa ajili ya uendelezaji wa miradi ya matumizi mengine.

**104. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2020/21, kazi zitakazotekelezwa ni kufanya maandalizi ya uchorongaji wa visima vya utafiti ili kuhakiki rasilimali ya jotoardhi kwa ajili ya uzalishaji wa umeme na kukamilisha uendelezaji wa miradi ya matumizi mengine katika eneo la Songwe. Katika mwaka 2020/21 jumla ya **Shilingi milioni 816.76** zimetengewa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo.

*(iii). Mradi wa Kiejo-Mbaka*

**105. Mheshimiwa Spika**, mradi huu unahusisha uzalishaji wa umeme wa **MW 10** na matumizi mengineyo katika maeneo ya Kiejo na Mbaka, mkoani Mbeya. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kukamilika kwa uainishaji wa maeneo ya kuchoronga visima vifupi kwa ajili ya mradi wa matumizi mengine; kumpata Mkandarasi wa uchorongaji na kukamilisha



uainishaji wa mahitaji ya ardhi kwa ajili ya mradi wa matumizi mengine.

**106. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21, kazi zilizopangwa ni: kukamilisha uchorongaji wa visima vifupi; kutekeleza mradi wa matumizi mengine; na kufanya maandalizi ya uchorongaji wa visima virefu vya utafiti. Jumla ya **Shilingi bilioni 4.53** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

### Shughuli za Udhhibiti wa Sekta Ndogo ya Umeme

**107. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia EWURA imeendelea kusimamia na kudhibiti utendaji wa mafundi umeme wanaofanya kazi za kuunganisha mifumo ya umeme majumbani, viwandani na sehemu za biashara. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Serikali kupitia EWURA imetoa leseni 782 kwa lengo la kuimarisha usalama wa wananchi na mali zao. Serikali kupitia Wizara ya Nishati inatoa rai kwa wananchi kutumia mafundi waliosajiliwa na kuacha kuwatumia mafundi wasiokuwa na leseni (vishoka).

**108. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia EWURA katika mwaka 2019/2020 vilevile, imeendelea kuweka mazingira stahiki ya kiudhibiti ili kuwezesha utekelezaji wa miradi na kufanya ukaguzi katika miundombinu ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme.

## SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ASILIA

### *Shughuli za Utafutaji, Uendelezaji, Uzalishaji na Usambazaji wa Mafuta na Gesi Asilia Nchini*

**109. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2019/2020 shughuli za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia nchini zimeendelea. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2020 takriban **Futi za Ujazo Trilioni 57.54** za gesi asilia zimegunduliwa. Kati ya kiasi hicho, gesi iliyogunduliwa nchi kavu ni **futi za ujazo Trilioni 10.41** na kwa upande wa kina kirefu cha bahari ni **futi za ujazo Trilioni 47.13**. Shughuli za uzalishaji zinafanyika katika vitalu viwili (2) vya Songo Songo na Mnazi Bay. Kiwango cha juu cha uzalishaji wa gesi asilia kimeongezeka kutoka **futi za ujazo milioni 95** kwa siku mwaka 2015/16 hadi **futi za ujazo milioni 210** kwa siku mwaka 2019/2020 sawa na **ongezeko la asilimia 121.05**. Kiasi hiki cha gesi kinatumika katika uzalishaji wa umeme, viwandani, majumbani, taasisi pamoja na kwenye magari.

**110. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia PURA imeendelea na udhibiti wa shughuli za mkondo wa juu zinazohusu utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu 11 nchini kupitia mikataba ya Uzalishaji na Ugawanaji Mapato (*Production Sharing Agreement - PSAs*). Vilevile, EWURA imeendelea kutunga kanuni ndogo (*rules*) na miongozo ya kuimarisha kazi ya udhibiti katika mkondo wa kati na wa chini wa mafuta na gesi ili kuboresha huduma zinazotolewa.

## UTAFUTAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA KATIKA VITALU VYA KIMKAKATI UNAOTEKELEZWA NA SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA (TPDC)

111. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kupitia TPDC imeendelea na utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya kimkakati vikiwemo Mnazi Bay Kaskazini na Eyasi – Wembere. Utekelezaji na mipango ya miradi ya utafutaji na uendelezaji mafuta na gesi asilia nchini katika eneo la Mnazi Bay na Eyasi Wembere ni kama ifuatavyo:

### (i). *Kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini*

112. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kupitia TPDC imepanga kuchoronga visima viwili (2) ambapo kisima kimoja ni cha utafutaji na kingine cha uhakiki. Uamuzi wa kuendeleza kitalu hiki umezingatia taarifa za awali katika eneo hilo zinazoonesha uwepo wa mashapo yenye uwezekano wa kuwa na gesi asilia. Kazi zilizotekelezwa mwaka 2019/20 ni pamoja na kukamilika kwa tathmini ya taarifa za kijiolojia na kijiiofizikia na kumpata Mtaalamu Mshauri wa uchorongaji (*Drilling Management Consultant*). Katika mwaka 2020/21, kazi zitakazofanyika ni pamoja na kuchoronga visima vya utafutaji na uhakiki na kukamilisha rasimu ya Mkataba kati ya Serikali na TPDC kuhusu utafutaji na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia katika kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini. Jumla ya **Shilingi bilioni 102** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo.

### (ii). *Kitalu cha Eyasi – Wembere*

113. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu umelenga kufanya shughuli za utafutaji wa mafuta katika kitalu cha Eyasi – Wembere kwa kufanya utafiti wa kijiolojia, kijiiofizikia na kijiokemia ili kujiridhisha kuhusu uwepo wa mafuta katika kitalu hicho. Shughuli za awali za utafiti zilizotekelezwa kwa mwaka 2019/20 ni pamoja na: kukamilisha uchorongaji wa visima viwili (2) vifupi katika maeneo ya Kining'inila-Igunga na Nyaranja-Meatu kwa kutumia wataalamu wa TPDC na STAMICO; kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira; na kutoa elimu kwa jamii kuhusu mradi.

114. *Mheshimiwa Spika*, Kwa mwaka 2020/21, kazi zitakazofanyika ni pamoja na: kuchoronga kisima kifupi cha utafutaji katika eneo la Luono - Singida; kukusanya, kuchakata na kutafsiri data za kijiokemia; kutayarisha moduli ya 3D ya *Airbone Gravity Gradiometry (AGG)*; kukamilisha taarifa za kimaabara za sampuli zilizokusanywa kutoka visima vitatu (3); kuendelea na Tathmini ya Athari kwa Mazingira na kukusanya data za mitetemo za 3D. Katika mwaka 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 500** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.



## MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA USAFIRISHAJI NA USAMBAZAJI GESI ASILIA

### (i) *Usambazaji wa Gesi Asilia kwa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani*

115. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unahusu ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani ambao utahusisha ujenzi wa miundombinu ya usambazaji kwa njia ya mabomba na gesi asilia iliyoshindiliwa (CNG) ambapo vituo vitano vitajengwa katika maeneo ya Chuo kikuu cha Dar es Salaam, Kituo cha mabasi Ubungo, Soko la Samaki Feri, Hospitali ya Taifa Muhimbili na Kibaha. Vituo hivi vitawezesha usambazaji wa gesi viwandani, kwenye magari na majumbani katika maeneo husika.

116. *Mheshimiwa Spika*, kazi zilizotekelezwa mwaka 2019/20 ni pamoja na: kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia (*trunk-lines*) yenye urefu wa kilomita 18 yenye uwezo wa kuunganisha zaidi ya wateja 10,000 wa majumbani katika Mkoa wa Dar es Salaam katika maeneo ya Sinza, Mlalakuwa, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Ubungo Msewe na nyumba za Polisi Kurasini. Hadi kufikia Aprili, 2020, jumla ya wateja wapatao 500 wa majumbani na viwanda 48 vimeunganishwa na gesi asilia. Vilevile, magari zaidi ya 400 yametumia gesi asilia hadi futi za ujazo milioni 11.1 kwa mwaka 2019 kutoka futi za ujazo milioni 1.9 kwa mwaka 2018, kiasi hiki ni **ongezeko la asilimia 500** ya matumizi ya gesi kwenye magari kulinganisha na mwaka 2018. Katika eneo la Mkuranga mkoani Pwani, miundombinu yenye urefu wa kilomita 6 yenye uwezo wa kuunganisha viwanda zaidi ya 20 imejengwa.

117. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa mradi wa CNG, maeneo yatakapojengwa miundombinu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Soko la Samaki Feri, Muhimbili na Kibaha yamepatikana; Usanifu wa kina wa kihandisi pamoja na Tathmini ya Athari kwa Mazingira vinaendelea. Mpango wa Serikali ni kuhakikisha mikoa mingi inanufaika na gesi asilia iliyogunduliwa Tanzania. Kwa kuanzia, TPDC ina mpango wa kusambaza gesi kwa kutumia CNG, Mini LNG na mabomba kwa mikoa ya Morogoro, Dodoma, Tanga, Arusha, Mwanza, Shinyanga, Kagera, Manyara, Geita na Kilimanjaro.

118. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/21, kazi zilizopangwa kufanyika katika Mkoa wa Pwani ni pamoja na: kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira; na kumpata Mkandarasi (*EPC contractor*) kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya usambazaji katika maeneo ya Mwanambaya na Mkiu. Vilevile, kazi nyingine zilizopangwa kufanyika katika Mkoa wa Dar es Salaam ni pamoja na kulipa fidia ya kutwaa ardhi kwa ajili ya maeneo yatakayowekwa mradi wa CNG katika maeneo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; kufanya Tathmini za Athari kwa Mazingira katika mkuza wa miundombinu pamoja na ujenzi wa bomba kutoka Mwenge hadi Mbezi Beach na kutoka Tegeta (Wazo Hills) hadi Bagamoyo. Serikali imetenga **Shilingi bilioni 1.1** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

*(ii) Usambazaji wa Gesi Asilia Mkoani Lindi na Mtwara*

119. Serikali kupitia TPDC inaendelea na kazi za kusambaza gesi asilia kwa wateja wote walio karibu na miundombinu ya usambazaji katika Mikoa ya Mtwara na Lindi. Kazi zilizotekelezwa mwaka 2019/20 ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya usambazaji gesi asilia (*trunk-lines*) yenye urefu wa Kilomita 17 yenye uwezo wa kuunganisha zaidi ya wateja 3,000 kwa Mkoa wa Mtwara katika maeneo ya Chuo cha Ufundi, Chuo cha Ualimu Mtwara, Sekondari ya Ufundi na Gereza la Lilungu na Mitaa ya Magomeni, Shangani, Reli, Chikongola na Tandika. Hadi sasa, nyumba 425 zimefikwa na miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia na uunganishaji unaendelea.

120. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/21, kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira katika mikoa ya Lindi na Mtwara; kumpata Mkandarasi (EPC contractor) kwa ajili ya ujenzi wa bomba lenye urefu wa Kilomita 7.8 kutoka kwenye bomba la usafirishaji gesi asilia hadi Mnazi Mmoja – Lindi; ununuzi wa Mtambo wa kupima kiwango cha gesi, kupunguza msukumo na kuweka harufu kwa ajili ya usalama (*Metering Pressure Reduction System and Odorization unit*); Mradi huu unalenga kujenga miundombinu ya usambazaji wa gesi asilia katika Manispaa ya Lindi kupitia Mnazi Mmoja ambapo takriban wateja wa awali zaidi ya 1,000 wataunganishwa. **Shilingi bilioni 10.1** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

*(iii) Mradi wa Kusafirisha Gesi Asilia kutoka Tanzania kwenda Uganda*

121. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unahusu ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Tanzania hadi Uganda, ambao utasambaza gesi asilia maeneo ya Tanzania yatakayopitiwa na bomba hilo. Katika mwaka 2019/20, kazi zilizotekelezwa ni pamoja: kuandaliwa kwa rasimu ya taratibu na kanuni za manunuzi; kukamilika kwa *Expression of Interest (EOI)* kwa ajili ya kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya Upembuzi Yakinifu wa mradi; kuandaliwa kwa kanuni zitakazoongoza Kamati ya Pamoja ya Wataalamu; na kuandaliwa kwa rasimu ya Makubaliano ya Pamoja (*Bilateral Agreement*) kati ya Serikali ya Tanzania na Uganda.

122. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2020/21 kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: kukamilisha kanuni na taratibu za manunuzi; kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya upembuzi yakinifu; na kufanya tafiti nyingine kwa ajili ya mradi. Jumla ya **Shilingi milioni 355.4** zimetengwa ili kutekeleza kazi hizo.

## MRADI WA KUCHAKATA NA KUSINDIKA GESI ASILIA (Liquefied Natural Gas – LNG)

123. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unalenga kusindika gesi asilia iliyogunduliwa katika eneo la kina kirefu cha bahari katika Vitalu Na. 1, 2 na 4 kuwa kimiminika ili iuzwe nje ya nchi na nyingine itumike ndani ya nchi. Kazi zilizotekelezwa kwa mwaka 2019/20



ni pamoja na: kuendelea kwa tafiti za namna ya kuzalisha na kusafirisha gesi kutoka bahari kuu hadi eneo la mradi; kuendelea na majadiliano ya Mikataba Hodhi (*Host Government Agreement - HGA*) baina ya Serikali na Kampuni za utafutaji na uendelezaji zitakazotekeleza mradi na ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha mradi. Jumla ya **shilingi bilioni 5.2** zimeanza kulipwa kuanzia mwezi Mei 2020 kwa wananchi wapatao 693 watakaopisha mradi. Katika mwaka 2020/21, kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: kuendelea na tafiti mbalimbali za kitaalam na kuendelea na majadiliano ya mradi. Jumla ya **Shilingi bilioni 2.6** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo.

## **UTEKELEZAJI WA MPANGO KABAMBE WA MATUMIZI YA GESI ASILIA (NATURAL GAS UTILIZATION MASTER PLAN – NGUMP)**

**124.** *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea na utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asilia (NGUMP) ambao unatoa mwongozo kuhusu matumizi bora ya gesi asilia, uboreshaji wa miundombinu ya gesi asilia pamoja na kuweka misingi ya kuhakikisha Sekta zote za uchumi zinanufaika na matumizi ya gesi asilia. Katika Mpango huo, jumla ya **Futi za Ujazo Trilioni 18.7** za gesi asilia zimepangwa kutumika kwa ajili ya matumizi ya soko la ndani katika uzalishaji umeme, viwandani, kuzalisha mbolea, majumbani, taasisi na magari.

**125.** *Mheshimiwa Spika*, katika kufanikisha utekelezaji wa NGUMP, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Japan kupitia JICA imeanzisha stadi za Mpango wa Kuhamasisha Matumizi ya Gesi Asilia Nchini (DNGPP). Mpango huo umeainisha matumizi ya teknolojia nafuu katika usambazaji wa gesi asilia hususan katika maeneo ambayo soko la gesi asilia bado ni changa. Teknolojia nafuu inayopendekezwa ni pamoja na matumizi ya gesi kimiminika iliyosindikwa na gesi iliyoshindiliwa (Mini-LNG & CNG) katika kusambaza gesi asilia maeneo mbalimbali nchini.

**126.** *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2019/20 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kuandaa Rasimu ya Mpango wa Kuhamasisha Matumizi ya Gesi Asilia Nchini (*Draft Domestic Natural Gas Promotion Plan – DNGPP*), uhakiki wa awali wa mahitaji ya gesi asilia nchini; uchambuzi wa awali wa kiuchumi na kiufundi wa teknolojia mbalimbali za usafirishaji na usambazaji wa gesi asilia; pamoja na uchambuzi wa awali wa Mradi wa mfano wa usambazaji gesi asilia katika Jiji la Dodoma.

**127.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/21 kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na: kufanya upembuzi yakinifu wa kina wa teknolojia zilizopendekezwa kwenye Mpango wa DNGPP; kuhakiki mahitaji ya gesi asilia nchini na kuhamasisha matumizi ya gesi asilia katika maeneo mbalimbali nchini; na kuanza hatua za awali za utekelezaji Mradi wa Mfano katika Jiji la Dodoma.

## MIRADI YA KUHIFADHI NA KUSAFIRISHA MAFUTA

### (i) *Uhifadhi na Biashara ya Mafuta*

128. *Mheshimiwa Spika*, Serikali imeendelea na taratibu za uanzishaji na usimamizi wa Hifadhi ya Kimkakati ya Mafuta ya Akiba ya Dharura na kushiriki katika biashara ya kuagiza na kuuza mafuta. Kazi zilizotekelezwa kwa mwaka 2019/20 ni pamoja na: kukamilika kwa stadi za biashara ya mafuta; kukamilika kwa usajili ili kuanza kuagiza mafuta; na kuanza taratibu za kutwaa maeneo ya kimkakati katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Morogoro na Dodoma.

129. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/21, kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na; kuendelea na utwaaji wa maeneo yaliyoainishwa, kuanza biashara ya mafuta na kulipa gharama mbalimbali za uendeshaji. Serikali kupitia TPDC imetenga **Shilingi bilioni 31.2** kutekeleza kazi hizo.

### (ii) *Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania (East African Crude Oil Pipeline)*

130. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu unahusu ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi (*crude oil*) kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania). Katika kipindi cha mwaka 2019/20 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kukamilika kwa kazi ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira; na kuendelea na utoaji wa elimu kwa umma kwa maeneo ya pembezoni mwa eneo la mradi.

131. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2020/21 kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: kukamilisha majadiliano ya mikataba ikiwemo ya Nchi Hodhi na Wawekezaji (HGA), Mkataba wa Ubia (SHA), Mkataba wa Bandari, Mkataba wa Pango la Ardhi (*Land Lease Agreement*) na kulipa fidia. Jumla ya **Shilingi bilioni 1** zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo. Mradi unatarajiwa kuanza mwezi Aprili, 2021 baada ya kufanyika kwa Maamuzi ya Mwisho ya Uwekezaji (*Final Investment Decision – FID*)

### (iii) *Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Safi (Refined Petroleum Products) kutoka Dar es Salaam (Tanzania) hadi Ndola (Zambia)*

132. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu umepangwa kutekelezwa kwa ushirikiano wa Serikali za Tanzania na Zambia. Mradi unahusu ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta safi kutoka Dar es salaam (Tanzania) hadi Ndola (Zambia) likiwa na matoleo ya mafuta (*take-off points*) katika maeneo ya Morogoro, Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe. Mradi huu utaiwezesha Serikali kuongeza mapato, ajira, kuongeza uhakika wa upatikanaji wa mafuta katika maeneo linapopita bomba, pamoja na kuepusha uharibifu wa miundombinu ya barabara, kupunguza gharama za usafirishaji wa mafuta na kupunguza msongamano wa magari jijini Dar es Salaam. Mradi utaongeza fursa za biashara katika ukanda wa nyanda za juu kusini.



133. *Mheshimiwa Spika*, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: kukamilika kwa andiko la awali la mradi; Hadidu za Rejea za Upembuzi Yakinifu na Athari kwa Mazingira na Kijamii pamoja na kupata ridhaa ya kufanyika kwa Upembuzi Yakinifu.

134. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2020/21, kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja kuendelea kukamilisha kumpata Mshauri Mwelekezi wa kufanya Upembuzi Yakinifu. Jumla ya **Shilingi milioni 500** zimetengwa kwa ajili ya kazi hizo.

## UDHIBITI WA SHUGHULI ZA MKONDO WA JUU WA MAFUTA NA GESI ASILIA

135. *Mheshimiwa Spika*, katika kutekeleza jukumu la kudhibiti shughuli za mkondo wa juu wa petroli kwa mwaka 2019/20, Serikali kupitia PURA imepitisha Mpango Kazi wa uchorongaji wa visima vinne (4) na uchukuaji wa data za mitetemo za 2D kilomita 450 za mstari na za 3D kilomita 717 za mraba. Aidha, PURA ilisimamia uchorongaji wa visima viwili vifupi (*stratigraphic boreholes*) katika maeneo ya Kining'inila na Nyaranja - Kitalu cha Eyasi Wembere. PURA imekamilisha ukaguzi na uhakiki wa gharama za uwekezaji, na mapato yatokanayo na uzalishaji wa gesi asilia kwa mwaka 2016 hadi 2018 na kuokoa zaidi ya **Shilingi Bilioni 10.14** ambazo mwekezaji aliziweka kama gharama za uwekezaji. Hatua hii imepelekea kuongezeka kwa pato la Serikali katika mgao wake wa uuzaji gesi asilia.

136. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/21, Serikali kupitia PURA itaendelea kusimamia na kudhibiti shughuli za mkondo wa juu wa petroli. Shughuli hizo ni pamoja na: uchorongaji wa kisima kimoja (1) cha utafutaji (Chikumbi-1) katika kitalu cha Ruvuma; visima viwili (2) vya utafutaji (Mruka-1 na Mtarawanda-1), kisima kimoja (1) cha uendelezaji (Mambakofi-2) katika kitalu cha Ruvu; na uchorongaji wa visima vya utafutaji na uhakiki katika kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini. Kwa mwaka 2020/21, Jumla ya **Shilingi bilioni 1.69** zimetengwa kwa ajili ya kutekeleza majukumu hayo.

## HALI YA UAGIZAJI NA UPATIKANAJI WA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI NCHINI

137. *Mheshimiwa Spika*, Mfumo wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (*Bulk Procurement System - BPS*) unaosimamiwa na Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (*PBPA*) umeendelea kutumika kuagiza mafuta ya petroli, dizeli, mafuta ya taa na mafuta ya ndege. Katika mwaka 2019 jumla ya lita **bilioni 6.15** ziliingizwa nchini ikilinganishwa na lita **bilioni 5.70** zilizoagizwa mwaka 2018 sawa na ongezeko la **asilimia 7.4**. Kati ya kiasi hicho, lita **bilioni 3.54** sawa na **asilimia 57.5** ya mafuta yote yaliyoagizwa yalikuwa ni mafuta kwa ajili ya matumizi ya hapa nchini na lita **bilioni 2.62**, sawa na **asilimia 42.5** yalikuwa kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nchi jirani.

138. *Mheshimiwa Spika*, muda wa kupakua mafuta kutoka kwenye meli umepungua kutoka wastani wa siku 30 hadi 60 kabla ya mwaka 2015 na kufikia wastani wa siku 1 hadi 3 kwa mwaka 2020. Aidha, kiasi cha mafuta ya ziada kimeongezeka kutoka lita milioni 185 mwaka 2018 hadi lita milioni 365 mwaka 2019 sawa na **ongezeko la asilimia 97.3**. Mafuta haya yanatosheleza wastani wa matumizi ya zaidi ya siku 40 kwa kila aina ya mafuta.

139. *Mheshimiwa Spika*, kiasi cha gesi ya mitungi (*Liquefied Petroleum Gas - LPG*) kilichoingizwa nchini kimeendelea kuongezeka ambapo kwa mwaka 2019 kilifikia **tani 166,436** ikilinganishwa na **tani 142,940** mwaka 2018 sawa na ongezeko la **asilimia 16.4**. Aidha, matumizi ya gesi hiyo nchini yameendelea kuongezeka ambapo kwa mwaka 2019 yalifikia **tani 106,301** ikilinganishwa na **tani 92,492** mwaka 2018 sawa na ongezeko la **asilimia 15**. Ongezeko hilo limechangiwa na juhudi mbalimbali za Serikali kwa kushirikiana na Kampuni zinazouza LPG katika kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kutumia LPG katika kutunza mazingira na kupunguza madhara ya kiafya yanayotokana na matumizi ya kuni na mkaa.

## MWENENDO WA BEI ZA MAFUTA

140. *Mheshimiwa Spika*, bei za mafuta katika soko la Dunia zimeendelea kushuka kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo uhitaji na upatikanaji wa bidhaa hii muhimu katika shughuli za kiuchumi. Wastani wa bei ya mafuta ghafi katika soko la dunia katika mwezi Aprili, 2020 ilifikia Dola za Marekani 23.27 kutoka Dola za Marekani 60.39 kwa pipa mwaka 2019 sawa na punguzo la asilimia 61.5.

141. *Mheshimiwa Spika*, kushuka kwa bei ya mafuta ghafi katika soko la Dunia kumesababisha kushuka kwa bei ya mafuta yaliyosafishwa ambapo wastani wa bei ya mafuta yaliyosafishwa katika soko la dunia ilikuwa **Dola za Marekani 593, 578 na 612** kwa tani kwa mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa/ndege mtawalia, ikilinganishwa na wastani wa **Dola za Marekani 646, 606 na 575** kwa tani kwa kipindi kama hicho mwaka 2018. Hii ni sawa na pungufu ya **asilimia 8 na asilimia 5** kwa mafuta ya petroli na dizeli mtawalia. Aidha, bei ya mafuta ya taa/ndege imeongezeka kwa **asilimia 6**.

142. *Mheshimiwa Spika*, kutokana na kushuka kwa bei ya mafuta ya petroli na dizeli katika soko la Dunia, bei za mafuta haya katika soko la ndani pia zilishuka. Kwa mwaka 2019, wastani wa bei za mafuta katika soko la ndani kwa mafuta yaliyopokelewa kupitia bandari ya Dar es Salaam ilishuka ikilinganishwa na wastani wa bei za mafuta katika kipindi hicho mwaka 2018. Wastani wa bei za mafuta kwa Mkoa wa Dar es Salaam kwa mwaka 2019 kwa lita moja ilikuwa kama ifuatavyo: Petroli **Shilingi 2,200**, Dizeli **Shilingi 2,159** na Mafuta ya Taa **Shilingi 2,114** wakati wastani wa bei za mafuta hayo kwa mwaka 2018 ilikuwa **Shilingi 2,318** mafuta ya Petroli, **Shilingi 2,229** kwa mafuta ya Dizeli na **Shilingi 2,188** kwa Mafuta ya Taa ambazo ni sawa na punguzo la **asilimia 5, 3 na 3** mtawalia. Aidha, kwa wakati wote bei ya Mafuta ya Ndege hapa nchini ni sawa na bei ya mafuta ya taa kabla



ya kodi na tozo za Serikali.

## UDHIBITI WA UBORA WA MIUNDOMBINU NA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI NA GESI ASILIA

143. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kupitia EWURA imeendelea kusimamia na kuhakikisha miundombinu ya mafuta inajengwa na kuendeshwa kwa kuzingatia viwango stahiki. EWURA pia imeendelea kutoa leseni kwa miundombinu ambayo inakidhi viwango ambapo katika kipindi cha Januari 2019 hadi Machi, 2020, imetoa jumla ya leseni 570 za aina mbalimbali na vibali 197 vya ujenzi wa miundombinu ya mafuta. Aidha, EWURA imetoa kibali kwa Kampuni ya Dangote- Mtwara kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha kujaza gesi asilia iliyoshindiliwa kwenye magari (*Compressed Natural Gas*) ili kuyawezesha magari ya kampuni hiyo kutumia gesi asilia.

144. *Mheshimiwa Spika*, upatikanaji wa mafuta vijijini umeendelea kusimamiwa na kuzipatia ufumbuzi changamoto zilizopo kutokana na uhaba wa vituo vya mafuta katika maeneo hayo. Katika mwaka 2019/20, Serikali imeandaa utaratibu utakaorahisisha uwekezaji katika vituo vya mafuta ambao utapunguza gharama za uwekezaji kwa vituo vya mafuta vijijini ili mafuta yaweze kusambazwa katika njia bora na salama. Vilevile, Serikali inaandaa utaratibu utakaorahisisha usambazaji wa gesi asilia na LPG kwa maeneo ya vijijini. Taratibu hizo zinatarajia kukamilika mwezi Juni, 2020.

145. *Mheshimiwa Spika*, Serikali kupitia EWURA imeendelea kusimamia ubora wa bidhaa za mafuta ya petroli zinazosambazwa na kuuzwa nchini. Katika kipindi cha mwaka 2019, EWURA ilipima sampuli 280 ambapo kati hizo, sampuli 30 sawa na **asilimia 10.3** hazikukidhi viwango na hatua stahiki za kisheria zilichukuliwa dhidi ya wafanyabiashara waliokutwa na mafuta ambayo hayakidhi viwango.

146. *Mheshimiwa Spika*, njia nyingine inayotumika kudhibiti ubora na ukwepaji wa kodi katika biashara ya mafuta ni uwekaji wa vinasaba (*molecular marker*) katika mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa yanayotumika hapa nchini. Utaratibu huu umesaidia kudhibiti uchakachujaji, ukwepaji wa kodi na kuimarisha ushindani katika biashara ya mafuta. Katika mwaka 2019, EWURA ilipima vinasaba kwenye mafuta kutoka katika vituo vya mafuta 718 na kati ya vituo hivyo, vituo 23 sawa na **asilimia 3.2** vilikutwa na mafuta ambayo hayakuwa na kiwango sahihi cha vinasaba kwa mujibu wa kanuni. Hatua stahiki zilichukuliwa dhidi ya wafanyabiashara ambao mafuta yao hayakuwa na kiwango sahihi cha vinasaba ikiwemo kutozwa faini na kufikishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa ajili ya kulipa kodi stahiki walizokwepa.

147. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/21 Serikali itaendelea kusimamia sekta ya mafuta nchini ili kuhakikisha uwepo wa mafuta ya kutosha, yenye ubora stahiki, miundombinu ya mafuta yenye kukidhi ubora, usalama na utunzaji wa mazingira pamoja na ushindani ulio sawa wakati wote.

## MIRADI YA KUJENGA UWEZO KATIKA SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ASILIA

### (i) *Mradi wa Usimamizi wa Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Rasilimali za Asili Tanzania*

148. *Mheshimiwa Spika*, Mradi huu ulianza kutekelezwa kuanzia mwezi Juni, 2017 na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2021. Gharama za mradi ni kiasi cha **Dola za Marekani milioni 29.54** ambapo Mfuko wa Maendeleo wa Afrika unachangia **Dola za Marekani milioni 26.59** sawa na **Shilingi bilioni 62.08** na Serikali ya Tanzania itachangia **Dola za Marekani milioni 2.95** sawa na **Shilingi bilioni 6.90**.

149. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/20 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na: ununuzi na kuanza ufungwaji wa skana ya kukagulia mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam; kukamilika kwa awamu ya kwanza ya uboreshaji wa mfumo wa kieletroniki wa uondoaji wa shehena bandarini na katika mipaka (*Electronic Single Window System*); kukamilika kwa ununuzi na ufungwaji wa mifumo ya ukusanyaji mapato; na kukamilisha ununuzi na ufungaji wa vifaa vya kuhifadhi data za petroli.

150. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/21 kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na: kukamilisha ufungwaji na kuanza kutumika skana ya kukagulia mizigo; kukamilisha awamu ya pili ya uboreshaji wa mfumo wa kieletroniki wa uondoaji wa shehena bandarini na mipakani; na kukamilisha stadi za: mifumo ya bei ya gesi asilia, mchango wa sekta ya gesi asilia kwenye uchumi, mahitaji ya gesi asilia nchini; pamoja na uanzishwaji wa kituo cha utunzaji taarifa za mkondo wa juu (*data centre*) cha PURA. Jumla ya **Shilingi bilioni 25.8** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizi.

### (ii) *Mradi wa Oil For Development Programme (OfD) - Institutional Cooperation In the Upstream Petroleum Sub-Sector*

151. *Mheshimiwa Spika*, mradi huu una lengo la kujengea uwezo Wizara na Taasisi za Serikali zinazohusika na masuala ya usimamizi wa mafuta na gesi asilia nchini ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi. Wanufaika wa mradi huu ni pamoja na Wizara ya Nishati, Wizara ya Fedha na Mipango, PURA, TPDC, TRA, NEMC, TASAC na OSHA kwa upande wa Tanzania Bara. Kwa upande wa Zanzibar ni, Wizara ya Ardhi, Maji, Nyumba na Nishati; ZPRA; ZPDC; ZEMA; ZMA; na DOSH. Pamoja na kuzijengea uwezo Wizara na Taasisi husika, Mradi huu pia unasaidia katika kuandaa kanuni na miongozo mbalimbali itakayoimarisha usimamizi katika sekta ya mafuta na gesi asilia. Mradi ulianza kutekelezwa mwaka 2017 na utakamilika Julai, 2020.

152. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2019/20 kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kuwajengea uwezo maafisa 61 kutoka taasisi husika katika maeneo ya utunzaji wa takwimu, masuala ya mazingira na usalama mahala pa kazi pamoja na usimamizi wa mapato yatokanayo na shughuli za mafuta na gesi asilia.



## USHIRIKI WA WATANZANIA KATIKA SEKTA NDOGO YA MAFUTA NA GESI ASILIA

153. *Mheshimiwa Spika*, katika kuhakikisha Watanzania wanashiriki kikamilifu katika shughuli za mafuta na gesi asilia nchini. Mwaka 2018 Serikali ilianzisha Kanzidata ya Watoa Huduma wa Ndani (*Local Suppliers and Service Providers Database - LSSP*). Hadi mwezi Aprili, 2020, jumla ya Kampuni za Watanzania na zile za ubia 457 zimesajiliwa kwenye Kanzidata hiyo.

## UIMARISHAJI WA MAWASILIANO KATI YA WIZARA NA JAMII

154. *Mheshimiwa Spika*, pamoja na majukumu mengine, Wizara imeendelea na kazi ya utoaji taarifa kwa wadau kupitia Televisheni, Magazeti na Redio. Aidha, utoaji wa taarifa unajumuisha kupitia Tovuti ya Wizara, mitandao ya kijamii ya Wizara ambayo ni *facebook*, *Twitter*, *Instagram* na YouTube pamoja na Jarida la Wizara ya Nishati linalotolewa kila mwezi.

155. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2019/20 Wizara iliendelea kutoa taarifa mbalimbali za miradi mikubwa inayotekelezwa chini yake ikiwemo miradi ya uzalishaji na usafirishaji umeme, miradi ya mafuta na usambazaji wa gesi asilia na miradi ya usambazaji umeme vijijini. Katika mwaka 2020/21 Wizara itaendelea kutoa taarifa mbalimbali katika maeneo muhimu ya miradi mikubwa inayotekelezwa chini ya Wizara.

## AJIRA NA MAENDELEO YA RASILIMALIWATU

156. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kusimamia maendeleo ya Watumishi wake pamoja na kutekeleza vema Muundo wake ulioidhinishwa mwaka 2018 kwa kujaza jumla ya nafasi 7 za Uongozi zilizokuwa wazi. Katika mwaka 2020/21 Wizara inatarajia kuwapandisha vyeo Watumishi 67, kuajiri Watumishi 14 na kujaza nafasi 3 za uteuzi. Vilevile, jumla ya watumishi 58 wamepangwa kuajiriwa katika Taasisi zilizo chini ya Wizara kama ifuatavyo: TPDC (25), REA (10), PURA (8) na PBPA (15).

157. *Mheshimiwa Spika*, kwa kutambua umuhimu wa kuwawezesha na kuwajengea uwezo Watanzania katika masuala mbalimbali ya mafuta na gesi asilia, Wizara imeendelea kushirikiana na Washirika wa Maendeleo kwa kuwapatia ufadhili wa masomo Watanzania katika Shahada ya Kwanza, Uzamili na Uzamivu ili kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na wataalamu wa kutosha katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia. Vilevile, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo wataalam kupitia Mpango wa Uendelezaji wa Rasilimaliwatu wa Wizara. Katika mwaka 2019/20, Watanzania 17 walipatiwa fursa ya ufadhili wa masomo kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China katika fani ya mafuta na gesi asilia. Wizara pia iliwajengea uwezo watumishi 9 na watumishi 104 katika mafunzo mbalimbali ya muda mrefu na muda mfupi mtawalia.

158. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/21, Watanzania 20 wanatarajiwa kwenda masomoni kupitia ufadhili wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China katika fani ya mafuta na gesi asilia. Aidha, Wizara itawezesha ufadhili wa mafunzo ya muda mrefu kwa Watumishi 12 na mafunzo ya muda mfupi kwa Watumishi 63.

## USHIRIKIANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA

159. *Mheshimiwa Spika*, kwa niaba ya Serikali napenda kuwashukuru Washirika wa Maendeleo na nchi wahisani ambao wameendelea kutoa michango yao katika kufanikisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara. Napenda kutambua mchango wa: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Benki ya Ushirikiano wa Kimataifa ya Japan (JBIC), United Bank for Africa (UBA); Economic Development Cooperation Fund (EDCF - Korea), Mfuko wa Uendelezaji Jotoardhi (Geothermal Risk Mitigation Facility - GRMF) pamoja na Taasisi na Mashirika ya: JICA (Japan), KfW (Germany), AFD (Ufaransa), Sida (Sweden), NORAD (Norway); Umoja wa Ulaya (EU), Benki ya Exim (China), Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Shirika la Maendeleo la Canada (CIDA) na USAID (Marekani).

160. *Mheshimiwa Spika*, pia natoa shukrani kwa Serikali za Nchi za Burundi, Canada, China, Iceland, Japan, Kenya, Norway, Uingereza, Sweden, Marekani, Urusi, Afrika Kusini, Korea Kusini, Malawi, Misri, Msumbiji, Sweden, Rwanda, Ufaransa, Uganda na Zambia kwa ushirikiano wao katika kuendeleza Sekta ya Nishati. Vilevile, nishukuru Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kwa ushirikiano katika masuala ya kikanda yanayohusu Sekta hii. Kwa kipindi cha mwaka 2020/21, *Serikali kupitia Wizara ya Nishati itaendelea kuimarisha ushirikiano na Washirika wa maendeleo na wadau wengine ili kuhakikisha kuwa Sekta ya Nishati inachangia katika kutimiza azma ya Serikali ya kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.*

## HITIMISHO

161. *Mheshimiwa Spika*, kupitia Bajeti ya Mwaka 2020/21 Wizara inalenga kutekeleza dhamira ya Serikali ya kuhakikisha kuwa inazalisha umeme wa kutosha, wa uhakika, na wa gharama nafuu. Vilevile, bajeti imelenga kuimarisha shughuli za utafutaji na biashara ya mafuta na gesi asilia pamoja na kuwezesha wananchi kunufaika na rasilimali hizo.

162. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/21, Wizara ya Nishati inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi trilioni 2.197** ikilinganishwa na **Shilingi trilioni 2.142** iliyotengwa kwa Mwaka 2019/20, sawa na ongezeko la **asilimia 2.5**.

163. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa liidhinishe bajeti ya jumla ya **Shilingi 2,196,836,774,000** kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Nishati na Taasisi zake. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama ifuatavyo:



- (i) **Shilingi 2,168,437,184,000** sawa na **asilimia 98.7** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo za maendeleo, **Shilingi 1,967,689,292,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 200,747,892,000** ni fedha za nje; na
- (ii) **Shilingi 28,399,590,000** sawa na **asilimia 1.3** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 15,025,821,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 13,373,769,000** kwa ajili ya mishahara (PE) ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

**164. Mheshimiwa Spika**, kwa unyenyekevu mkubwa sana naomba tena nitoe shukrani zangu za dhiti kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara kwa anuani ya [www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz). Vilevile, Hotuba hii ina vielelezo mbalimbali ambavyo vimeambatishwa kwa ajili ya ufafanuzi wa masuala muhimu yanayohusu Sekta ya Nishati.

**165. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**VIELELEZO VYA HOTUBA YA MWAKA 2020/21  
KUHUSU SEKTA ZA NISHATI**

**1.0 UMEME NA NISHATI JADIDIFU**

**Kielelezo Na. 1: Uwezo wa mitambo ya Kufua Umeme  
Nchini Mwezi Aprili, 2020**

Na.	Jina la Kituo	Uwezo (MW)
1.	Kidatu	204.00
2.	Kihansi	180.00
3.	Mtera	80.00
4.	New Pangani Falls	68.00
5.	Hale	21.00
6.	Nyumba ya Mungu	8.00
7.	Uwemba	0.84
8.	Mwenga	4.00
9.	Yovi	0.95
10.	Matebmwe	0.59
11.	Darakuta	0.32
12.	Andoya	1.00
13.	Tulila	5.00
<b>Jumla Ndogo - Maji</b>		<b>573.70</b>
14.	Songas	189.00
15.	Ubungo I	102.00
16.	Tegeta	45.00
17.	Ubungo II	129.00
18.	Kinyerezi I	150.00
19.	Kinyerezi II	248.22
20.	Mtwara	22.00
21.	Somanga	7.50
<b>Jumla Ndogo - Gesi</b>		<b>892.72</b>
22.	Zuzu	7.40
23.	Nyakato	63.00
24.	Biharamulo	4.14
25.	Songea	7.67
26.	Namtumbo	0.34
27.	Ludewa	1.27
28.	Mbinga	2.00

29.	Madaba	0.48
	Ngara	2.50
<b>Jumla Ndogo - Mafuta</b>		<b>88.80</b>
30.	TAWNWAT	1.50
31.	TPC	9.00
<b>Jumla Ndogo - Biomass</b>		<b>10.50</b>
<b>Jumla Kuu</b>		<b>1,565.72</b>

Chanzo: TANESCO

**Kielelezo Na. 2: Njia za Kusafirisha Umeme na Vituo vya  
Kupoza Umeme**

Na.	Njia za Usafirishaji Umeme	Urefu (km)	
		Juni, 2015	Desemba, 2019
1.	Njia kuu za msongo wa 400 kV	-	670
2.	Njia kuu za msongo wa 220 kV	2,760.70	2,940.7
3.	Njia kuu za msongo wa 132 kV	1,549.00	1,697.47
4.	Njia kuu za msongo wa 66 kV	543.00	543
<b>Jumla</b>		<b>4,852.70</b>	<b>5,851.17</b>

Chanzo: TANESCO

Na.	Njia za Usambazaji Umeme	Urefu (km)	
		Juni, 2015	Desemba, 2019
1.	33kV	15,165.77	38,096.52
2.	11kV	5,387.01	6,705.12
3.	0.4kV	40,822.98	86,199.37
<b>Jumla</b>		<b>61,373.76</b>	<b>131,001.01</b>

Chanzo: TANESCO

**Kielelezo Na. 3: Orodha ya Miradi itakayofikisha MW 10,000**

MWAKA	JINA LA MRADI (MW)	UWEZO WA UZALISHAJI (MW)	MAHITAJI YA NCHI (MW)
2019	Existing	1,565.72	1,120
2020	Kinyerezi I Extension (185 MW)	1751	1,435
2021	• Rusumo (27 MW) • Murongo/Kikagati (7 MW)	1,785	1,629
2022	JNHPP (2115 MW)	3,900	2,036
2023	• Kakono (87 MW) • Solar IPP (150 MW)	4,137	2,329

2024	<ul style="list-style-type: none"> <li>Ruhudji (358 MW)</li> <li>Rumakali (222 MW)</li> <li>Wind (200 MW)</li> </ul>	4,917	2,677
2025	<ul style="list-style-type: none"> <li>Mtwara Gas (300 MW)</li> <li>Coal IPP (600 MW)</li> <li>Ngozi (Jotoardhi) (60 MW)</li> </ul>	5,577	3,053
2026	<ul style="list-style-type: none"> <li>Maragalasi (45 MW)</li> <li>Kikonge (300 MW)</li> </ul>	6,222	3,439
2027	Somanga Fungu (330 MW)	6,552	
2028	<ul style="list-style-type: none"> <li>Mpanga (160 MW)</li> <li>Kinyerezi III (600 MW)</li> <li>Kinyerezi IV (330 MW)</li> </ul>	7,642	3,850
2029	<ul style="list-style-type: none"> <li>Masigira (118 MW)</li> <li>Kiwira (400 MW)</li> </ul>	8,160	4,323
2030	<ul style="list-style-type: none"> <li>Ngaka (400 MW)</li> <li>Natron (Jotoardhi) (100 MW)</li> </ul>	8,660	4,878
2031	<ul style="list-style-type: none"> <li>Somanga Fungu II (300 MW)</li> <li>Songwe (180 MW)</li> <li>Solar Dodoma (60 MW)</li> </ul>	9,200	5,488
2032	<ul style="list-style-type: none"> <li>Ikondo Mnyera (340 MW)</li> <li>Mchuchuma (600 MW)</li> <li>Kiejo (Jotoardhi) (60 MW)</li> </ul>	10,200	6,177
<b>JUMLA</b>		<b>10,200</b>	<b>6,177</b>

Chanzo: Wizara ya Nishati, 2020

**Kielelezo Na. 4 : Wilaya na Halmashauri ambazo Vijiji vyake vimefikwa na Umeme hadi mwezi Machi, 2020**

NA.	MKOA	WILAYA/HALMASHAURI
1.	Iringa	Iringa Vijijini
2.	Iringa	Mafinga (M)
3.	Mbeya	Busokela
4.	Mbeya	Chunya
5.	Mara	Musoma Vijijini
6.	Mara	Butiama
7.	Mara	Bunda
8.	Pwani	Bagamoyo
9.	Pwani	Rufiji
10.	Pwani	Mafia
11.	Kilimanjaro	Mwanga
12.	Kilimanjaro	Rombo
13.	Kilimanjaro	Moshi
14.	Kilimanjaro	Siha
15.	Kilimanjaro	Hai
16.	Kilimanjaro	Same
17.	Dodoma	Dodoma (M)
18.	Dodoma	Kongwa
19.	Dodoma	Bahi
20.	Kagera	Misenyi
21.	Kagera	Karagwe
22.	Geita	Chato
23.	Mtwara	Masasi
24.	Mtwara	Tandahimba
25.	Tanga	Pangani
26.	Mwanza	Misungwi
27.	Mwanza	Sengerema
28.	Mwanza	Buchosa
29.	Shinyanga	Shinyanga (M)
30.	Shinyanga	Ushetu
31.	Kigoma	Buhigwe
32.	Morogoro	Kilombero
33.	Ruvuma	Madaba
34.	Arusha	Arusha
35.	Arusha	Meru
36.	Katavi	Mlele

**2.0 MAFUTA NA GESI ASILIA**

**Kielelezo Na. 5: Idadi ya Vituo vya Mafuta Nchini tangu Aprili, 2019 hadi 30 Machi, 2020**


Mkoa	Jumla ya Vituo vya Mafuta Tarehe 30 Aprili 2019	Jumla Ya Vituo Vya Mafuta Hadi Tarehe 31 Machi 2020	Ongezeko/Pungufu
Arusha	98	105	7
Coast	104	102	-2
Dar es Salaam	220	237	17
Dodoma	64	79	15
Geita	60	61	1
Iringa	35	37	2
Kagera	65	75	10
Katavi	11	13	2
Kigoma	39	46	7
Kilimanjaro	92	98	6
Lindi	25	36	11
Manyara	50	51	1
Mara	56	56	0
Mbeya	64	73	9
Morogoro	71	80	9
Mtwara	36	43	7
Mwanza	89	95	6
Njombe	32	37	5
Rukwa	18	18	0
Ruvuma	37	38	1
Shinyanga	59	64	5
Simiyu	28	29	1
Singida	22	31	9
Songwe	29	33	4
Tabora	31	40	9
Tanga	65	69	4
<b>Jumla ya Vituo</b>	<b>1,500</b>	<b>1,646</b>	<b>146</b>

Chanzo: EWURA

**Kielelezo Na. 6: KIASI CHA GESI ASILIA KILICHOTUMIKA KATIKA STANDARD CUBIC FEET (SCF)**

Mwaka	Uzalishaji Umeme	Viwandani	Taasisi	Majumbani	Magari
2015	28,970,831,027	2,896,763,103	11,279,413	505,755	111,944
2016	40,801,064,876	3,251,131,575	9,694,726	582,685	172,106
2017	41,939,359,983	2,843,910,549	10,102,609	605,446	519,717
2018	49,197,581,728	4,741,850,802	11,460,809	653,293	1,934,665
2019	55,492,033,578	4,766,429,347	11,981,176	689,726	11,124,014
<b>JUMLA</b>	<b>216,400,871,193</b>	<b>18,500,085,377</b>	<b>54,518,733</b>	<b>3,036,905</b>	<b>13,862,446</b>

Chanzo: TPDC



Chanzo: TPDC



**Kielelezo Na. 7: KIASI CHA GESI ASILIA KILICHOTUMIKA KATIKA STANDARD CUBIC FEET (SCF)**

Mwaka	Uzalishaji Umeme	Viwandani	Taasisi	Majumbani	Magari
2015	28,970,831,027	2,896,763,103	11,279,413	505,755	111,944
2016	40,801,064,876	3,251,131,575	9,694,726	582,685	172,106
2017	41,939,359,983	2,843,910,549	10,102,609	605,446	519,717
2018	49,197,581,728	4,741,850,802	11,460,809	653,293	1,934,665
2019	55,492,033,578	4,766,429,347	11,981,176	689,726	11,124,014

Chanzo: TPDC

**Kielelezo Na. 8: MABOMBA YA KUSAMBAZA GESI ASILIA NCHINI**

Mkoa	Jina	Umbali
Mtwara	1 Dangote awamu 1	2.70 km
	2 Dangote awamu 2	0.10 km
	3 Majumbani awamu 1	16.60 km
	<b>Jumla</b>	<b>19.40 km</b>
Pwani	1 GoodWill	1.65 km
	2 Lodhia	3.70 km
	3 Knauf	0.20 km
	<b>Jumla</b>	<b>5.55 km</b>
Dar es Salaam	1 Ubungo - Mikocheni	7.20 km
	2 NNGI - Ubungo Mikocheni	1.44 km
	3 Mitambo ya kuzalisha umeme	6.50 km
	4 Coca Cola	0.10 km
	5 Majumbani UDMSM	5.02 km
	6 Majumbani - Mikocheni	4.30 km
	7 Viwandani	53.00 km
	<b>Jumla</b>	<b>77.56 km</b>
<b>Jumla Kuu</b>	<b>102.51 km</b>	

Chanzo: TPDC

**Kielelezo Na. 9: FEDHA ZA KIGENI ZILIZOOKOLEWA KATIKA UCHUMI KWA KUTUMIA GESI ASILIA BADALA YA MAFUTA YANAYOAGIZWA NJE YA NCHI**

Na	SEKTA	Desemba 2015	Desemba 2019
		USD	USD
1	Majumbani, Taasisi na Magari	314,636	477,166
2	Viwandani	712,765,150	1,503,840,452
3	Uzalishaji Umeme	7,288,934,771	12,513,118,320
	<b>Jumla</b>	<b>8,002,014,557</b>	<b>14,017,435,938</b>

Chanzo: TPDC

**Kielelezo Na. 10: ORODHA YA VIWANDA VILIVYOUNGANISHWA NA MIUNDOBINU YA GESI ASILIA**

NA.	ORODHA YA VIWANDA
	Aluminium Africa-ALAF
	A-One Products & Bottlers Ltd
	Azam Bakeries Co. Ltd.
1.	Bautech Company Limited -1
2.	Bora Industries Limited
3.	Dar Brew
	East Coast Oils & Fats Ltd.
4.	Gaia Eco Solutions (Yuasa)
5.	Iron & Steels
6.	Kamal Steel Ltd
7.	Kioo Ltd (Kioo Generator, Kioo Furnace 1 & Kioo Furnace 2)
8.	MM Integrated Steel Mills (MMI 1)
9.	MM Integrated Steel Mills (MMI 2)
10.	MM Integrated Steel Mills (MMI 3)
11.	Murzah 1
12.	Murzah 2
13.	Murzah 3
14.	Murzah 4
15.	Namera Group of Industries Ltd.

NA.	ORODHA YA VIWANDA
16.	Nampak Industries
17.	Nida Textile Mills Tanzania Ltd.
18.	OK Plastic Limited
19.	Royal Soap & Detergent Industries
20.	Said Salim Bakhresa & Company Ltd.
21.	SBC (T) Limited (PEPSI)
22.	Serengeti Breweries Limited
23.	SILAFRICA TANZANIA LTD/Simba plastics Company
24.	Soap and Allied Industries Limited
25.	Steel Masters Ltd
26.	Tanpack Tissues Limited
27.	Tanzania Breweries Ltd & Dar Brew
28.	Tanzania Cigarette Company Ltd (TCC)
29.	Tanzania Cuttleries Manufactures Limited
30.	Tanzania-China Textile
31.	Tanzania Portland cement Company (TPCC)
32.	TCFTC (Urafiki Textiles)
33.	VOT Tanzania Ltd
34.	Yuasa batteries/GAIA ECO Solutions
35.	Simba steel/ Lakhani
36.	Karibu Textile
37.	Edible Oil
38.	Bautech Company Limited -2
39.	Goodwill ceramic
40.	Goodwill Packaging Factory
41.	Dangote Industries Tanzania Limited
42.	Coca-Cola Kwanza Limited
43.	Lodhia Steel
44.	Knauf Gypsum

Chanzo: TPDC

**Kielelezo Na. 11: Kiasi cha Gesi itokanayo na Petroli (LPG) iliyoagizwa Kuanzia Januari 2019 hadi Desemba 2019**

MWEZI	Kiasi cha LGP Kilichoagizwa (Tani)
Januari 2019	13,850
Februari 2019	11,868
Machi 2019	5,092
Aprili 2019	14,008
Mei 2019	15,395
Juni 2019	8,874
Julai 2019	20,088
Agosti 2019	16,988
Septemba 2019	17,067
Oktoba 2019	21,274
Novemba 2019	8,978
Desemba 2019	12,954
<b>Kiasi Kilichoagizwa 2019</b>	<b>166,436</b>
<b>Kiasi Kilichoagizwa 2018</b>	<b>142,940</b>
<b>Asilimia ya Mabadiliko</b>	<b>16%</b>

Chanzo: EWURA

**Kielelezo Na. 12: Mwenendo wa Bei za Mafuta katika Soko la Dunia na hapa nchini 2015-2019**

Mwaka	Wastani wa Bei ya Mafuta Katika Soko la Dunia			Wastani wa Bei ya Mafuta hapa nchini			
	Petroli (Tsh/Lita)	Dizeli (Tsh/Lita)	Mafuta ya Taa/Ndege (Tsh/Lita)	Petroli (Tsh/Lita)	Dizeli (Tsh/Lita)	Mafuta ya Taa (Tsh/Lita)	Mafuta ya Ndege (Tsh/Lita)
2015	832	795	792	1,973	1,808	1,739	1,064
2016	745	692	704	1,845	1,673	1,644	969
2017	893	906	887	2,004	1,873	1,832	1,117
2018	1,110	1,183	1,159	2,318	2,229	2,188	1,473
2019	1,013	1,103	1,075	2,200	2,159	2,114	1,399

Chanzo: PBPA na EWURA

**Kielelezo Na. 13: Mwenendo wa Uagizaji wa Mafuta toka 2015 hadi sasa Desemba 2019**

Mwaka	Mafuta yaliyoagizwa kwa Matumizi ya Ndani	Mafuta yaliyoagizwa kwa Matumizi ya Nje	JUMLA
2015	3,338,097,164	1,825,467,870	5,163,565,034
2016	3,302,298,898	2,185,151,066	5,487,449,964
2017	3,193,252,759	2,168,192,874	5,361,445,632
2018	3,264,785,479	2,440,025,165	5,704,810,644
2019	3,537,891,891	2,615,679,703	6,153,571,595

Chanzo: PBPA na EWURA

**Kielelezo Na.14: Mafuta yaliyoagizwa nchini kwa kipindi cha kuanzia Januari 2019 mpaka Desemba 2019 kwa matumizi ya ndani (katika Lita)**

MWEZI	DIZELI	PETROLI	MAFUTA YA TAA	MAFUTA YA NDEGE	MAFUTA MAZITO	JUMLA
Januari 2019	107,747,828	164,422,297	3,803,282	11,771,020		287,744,426
Februari 2019	228,055,234	92,909,535	1,752,820	13,857,846	2,009,201	338,584,636
Machi 2019	135,843,451	81,199,751	-	-	4,576,169	221,619,371
Aprili 2019	158,197,975	75,736,794	1,346,832	12,805,373		248,086,974
Mei 2019	142,273,191	79,844,652	3,654,979	23,054,946		248,827,768
Juni 2019	154,402,230	97,255,019	2,635,703	14,491,367		268,784,320
Julai 2019	156,915,925	98,840,307	6,872,312	19,357,559	9,046,851	291,032,955
Agosti 2019	167,784,459	98,129,488	1,905,888	18,971,736		286,791,570
Septemba 2019	151,994,286	84,436,914	1,423,603	20,942,981	2,590,494	261,388,278
Oktoba 2019	186,090,508	127,072,547	1,832,803	23,005,874		338,001,732
Novemba 2019	205,912,788	139,336,380	3,345,270	23,749,707		372,344,145
Desemba 2019	157,632,234	88,370,932				246,003,166
Jumlisha: Mafuta yaliyobadilishwa matumizi (Localized)	68,183,526	51,747,956	6,924,033	211,700	1,615,335	128,682,550
<b>Jumla mwaka 2019</b>	<b>2,021,033,634</b>	<b>1,279,302,572</b>	<b>35,497,526</b>	<b>182,220,109</b>	<b>19,838,051</b>	<b>3,537,891,891</b>
<b>Jumla mwaka 2018</b>	<b>1,801,701,249</b>	<b>1,194,245,131</b>	<b>27,279,769</b>	<b>220,994,910</b>	<b>20,564,420</b>	<b>3,264,785,479</b>
<b>Asilimia ya Mabadiliko</b>	<b>12.2%</b>	<b>7.1%</b>	<b>30.1%</b>	<b>-17.5%</b>	<b>-3.5%</b>	<b>8.4%</b>

Chanzo: EWURA



**Kielelezo Na. 15: Mafuta yaliyoagizwa nchini kwa kipindi cha kuanzia Januari 2019 mpaka Desemba 2019 kwa ajili ya kwenda nchi jirani (Transit) (katika Lita)**


MWEZI	DIZELI	PETROLI	MAFUTA YA NDEGE / TAA	MAFUTA MAZITO	JUMLA
Januari 2019	90,930,094	109,509,074	14,657,666	-	215,096,834
Februari 2019	205,448,686	92,955,998	15,290,204	6,830,287	320,525,175
Machi 2019	142,473,616	83,098,431	-	-	225,572,047
Aprili 2019	122,028,524	66,013,729	18,731,342	-	206,773,595
Mei 2019	140,815,098	54,227,574	26,361,930	-	221,404,602
Juni 2019	91,986,620	66,205,093	9,553,177	-	167,744,890
Julai 2019	105,487,114	63,041,340	11,005,880	1,030,754	180,565,088
Agosti 2019	122,609,760	79,948,342	12,066,008	-	214,624,110
Septemba 2019	127,332,458	70,482,203	14,737,061	-	212,551,722
Oktoba 2019	181,925,996	89,546,564	18,086,301	-	289,558,861
Novemba 2019	154,278,440	89,992,812	15,268,937	-	259,540,189
Desemba 2019	159,888,697	68,901,108			228,789,805
Kutoa - Mafuta yaliyobadilishwa matumizi (Localized)	68,183,526	51,747,956	7,135,732	-	127,067,215
<b>Jumla mwaka 2019</b>	<b>1,577,021,578</b>	<b>882,174,312</b>	<b>148,622,773</b>	<b>7,861,041</b>	<b>2,615,679,703</b>
<b>Jumla mwaka 2018</b>	<b>1,446,066,928</b>	<b>795,475,532</b>	<b>191,128,498</b>	<b>7,354,206</b>	<b>2,440,025,165</b>
<b>Asilimia ya Mabadiliko</b>	<b>9.1%</b>	<b>10.9%</b>	<b>-22.2%</b>	<b>6.9%</b>	<b>7.2%</b>

Chanzo: EWURA

**Kielelezo Na. 16: Mwenendo wa uagizaji wa mafuta kwa ajili ya matumizi ya ndani na nje kwa kipindi cha kuanzia Januari 2019 mpaka Desemba 2019**


	Mafuta yaliyoagizwa kwa Matumizi ya Ndani	Mafuta yaliyoagizwa kwa Matumizi ya Nje	JUMLA
2018	3,264,785,479	2,440,025,165	5,704,810,644
2019	3,537,891,891	2,615,679,703	6,153,571,595
Asilimia ya Mabadiliko	8.4%	7.2%	7.9%
Matumizi ya Ndani dhidi ya Matumizi ya Nje mwaka 2018	57.2%	42.8%	100%
Matumizi ya Ndani dhidi ya Matumizi ya Nje mwaka 2019	57.5%	42.5%	100%

Chanzo: EWURA




**Mchoro Na. 1: Mwenendo wa kiasi cha mafuta yaliyoingizwa nchini kwa ajili ya matumizi ya ndani na yaliyokwenda nchi jirani kwa kipindi kinachoanzia Januari 2019 mpaka Desemba 2019**

**Mchoro Na. 2: Mwenendo wa Uagizaji wa Mafuta toka 2015 hadi sasa Desemba 2019**




Chanzo: PBPA na EWURA

**Mchoro Na. 3: MAFUTA YALIYOINGIZWA NCHINI MWAKA 2019 KWA MATUMIZI YA NDANI YA NCHI**



Chanzo: PBPA

**Mchoro Na. 4: MAFUTA YALIYOINGIZWA NCHINI MWAKA 2019 KWENDA NCHI JIRANI**



Chanzo: PBPA





## LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI

# WIZARA YA NISHATI

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, 40474 Dodoma

 Wizara ya Nishati  Wizara\_ya\_nishati\_tanzania  
 @nishati2017  Wizara ya Nishati  [www.nishati.go.tz](http://www.nishati.go.tz)

